

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Tisa - Tarehe 16 Novemba, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti(Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu

NDG.JOSHUA CHAMWELA-KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Nchini ya mwaka wa fedha 2017.

MWENYEKITI: Ahsante. Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

Na. 106

Ujenzi wa Barabara za Vijiji - Sumbawanga Vijijini

MHE. IGNAS A. MALOCHA aliuliza:-

Barabara za vijiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga Vijijini zimekuwa ni kikwazo kikubwa cha kufanya wananchi washindwe kuuza mazao yao na hivyo kuendelea kuwa maskini.

(a) Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kujenga barabara ya Kaengesa - Kitete, Ilembo - Ntumbi - Itela na Kavifutu - Laela?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kujenga Daraja la Kaengesa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Jimbo la Kwela lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kaengesa - Chitete-Chisungamile yenye urefu wa kilometa 13.5 inaunganisha Vijiji, Kata, Wilaya ya Sumbawanga na Wilaya ya Kalambo. Barabara ya Ilembo - Ntumbi - Itela yenye urefu wa kilometa 17.3 inaunganisha vijiji, kata na inaunga kwenye barabara kuu inayokwenda Makao Makuu ya Wilaya ya Sumbawanga. Barabara aya Kavifutu - Laela yenye urefu wa kilometa 12 inaunganisha vijiji, kata na barabara kuu inayokwenda Makao Makuu ya Wilaya ya Sumbawanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Barabara za Mijini na Vijiji kwa maana ya *TARURA* imefanya tathmini ya ufunguzi na matengenezo ya barabara hizi ili kuzifanya zipitike muda wote. Kiasi cha shilingi bilioni 1.5 zinahitajika ili kukamilisha kazi hiyo. *TARURA* itafanyakazi hiyo kwa awamu na itazipa kipaumbele kwa kuzitengea fedha kwenye bajeti zake zijazo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile *TARURA* ilifanya tathmini ya Daraja la Kaengesa na kiasi cha shilingi milioni

320 kinahitajika. *TARURA* italipa kipaumbele Daraja la Kaengesa kwa utenga bajeti ya ujenzi kwenye bajeti zake zijazo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Malocha.

MHE. IGNAS A. MALOCHA:Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kaengesa - Chitete - Kisungamile, barabara ya Ilembu - Ntumbi - Tela na barabara ya Kavifuti - Laela zimejifunga sasa ni mwaka wa pili Serikali haijapeleka hela na maeneo hayo ni maeneo ya uzalishaji, kwa hiyo wananchi wako kisiwani. Nataka Serikali iniambie ni lini watapeleka fedha *TARURA* ili barabara hizi ziweze kujengwa kwa wakati?

Swali la pili, Daraja la Kaengesa ni daraja lililojengwa na Wamisionari, lilibebwa na mvua yapata miaka minne sasa hivi ni adha kubwa kwa wanafunzi, watumishi, mapadri na wananchi wanaozunguka vijiji vya maeneo hayo. Nataka Serikali iniambie ni lini sasa itapeleka fedha ili daraja hilo lijengwe?

MWENYEKITI: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu kwanza nichukue fursa hii kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha jinsi ambavyo amekuwa akipigania barabara katika Jimbo lake ukianza kwenda Rukwa Bondeni na Ukanda wa juu wa Ufipa hakika anastahili pongezi. Lakini katika maswali yake mawili ana shauku kubwa ya kutaka kujua ni lini barabara hizi zitaweza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kwanza kumuelekeza Meneja wa *TARURA* kuhakikisha

kwamba katika fedha ambazo zimepatikana baada ya kwamba kumekuwa na *exempt* kwenye VAT, fedha hizo ambazo zimeokolewa zielekezwe kwenda kuhakikisha kwamba matatizo haya ambayo Mheshimiwa Mbunge anayasema yanakwenda kutatuliwa kwa sababu adhama ya Serikali ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na *exempt* kwenye VAT. Zile fedha zinazopatikana zikatatue matatizo kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameyesema kuhusian an Jimbo lake.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Marangu Mtoni - Mshihiri mpaka Babylon yenye kilometa 9.2 ilitakiwa kufunguliwa na itagharimu zaidi ya shilingi milioni 450 ambapo kupitia mfuko wa maendeleo wa *Vunjo Development Foundation* wamekusanya wadau mbalimbali na Mbunge akiwepo na wananchi tumeshachanga zaidi ya shilingi milioni 200 kutengeneza barabara hii bado shilingi milioni 250 na kazi imeshaanza. Serikali inaji-*commit* kiasi gani cha kuongezea kwenye barabara hii ambapo kupitia motisha, nguvu za wananchi?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo wangu kwanza naomba uniruhusu nimpongeze ndugu yangu Mbatia ni miongoni mwa Wabunge ambao wamepata fursa ya kwenda kuonana na Mheshimiwa Rais akiwa anatokea upande wa pili na yeye siku zote amekuwa akisisitiza kwamba maendeleo hayana vyama.

Naomba niwapongeze wananchi ambao wamejitolea kwa kuchanga hicho kiasi cha shilingi milioni 200. Ni vizuri hicho kiasi cha fedha ambacho kimeshachangwa kikaanza kutumika na sisi kama Serikali tutakuwa tayari kuhakikisha kwamba hayo mapungufu mengine tunaongezea ili wananchi waweze kupata huduma.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti maalum na linaelekeza Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 107

Fedha za Ujenzi wa Wodi - Namtumbo

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo ina miaka mitano tangu ilipokamilisha ujenzi wa jengo la *OPD* lakini mpaka sasa hakuna uendelezaji wa ujenzi wa wodi yoyote ile na hakuna fedha yoyote inayopelekwa kwa ajili ya ujenzi huo.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha iliyotengwa katika bajeti kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi huo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo ulianza mwaka 2010/2011 ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliyoitoa mwaka 2009.

Mheshimiwa Mweenyekiti, jumla ya fedha ambayo Serikali ilikwishapeleka kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo kuanzia mwaka wa fedha 2010/2011 hadi 2012/2013 ni shilingi milioni 600.

Vilevile mwaka wa fedha 2017 Halmashauri ilianzisha harembee itwayo *Namtumbo Selous Marathon* ili kutafuta fedha za kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na ilifanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi 260,634,000 kilichotumika kununua vifaa tiba na kuendeleza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo ni miongoni mwa hospitali 67 za Wilaya zinazojengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 100.5 na tayari Serikali imeshapeleka shilingi 500 mwezi Oktoba, 2018 kwenye Halamshauri ya Wilaya ya Namtumbo kwa ajili ya kuanza ujenzi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Msongozi.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niipongeze sana Serikali kwa kuona umuhimu wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wote siyo wakati wa kuilaumu Serikali lakini mimi nimesimama leo niipongeze kwa sababu Serikali baada ya kuona changamoto hii, imepeleka fedha shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa wodi na *theatre* ya akina mama. Lakini pia nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wananamtumbo na wadau mbalimbali akiwemo Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson ambae alikuja katika Wilaya yetu na...

MWENYEKITI: Unaonaje ukiuliza maswali?

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:...kama mgeni rasmi na kuchangisha fedha shilingi milioni 260.

MWENYEKITI: Swali sasa.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Kwa hiyo, swali langu jambo moja ambalo nilikuwa napenda kulisema kwa maana ya swali sasa, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Hospitali hii ya Wilaya ili wananchi wa Wilaya ya Namtumbo waweze kupata huduma kwa haraka?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo wangu naomba kwa ujumla na mimi nipongeze wananchi wa Namtumbo pamoja na Mbunge wa Viti Maalum kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakipigania kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma iliyo bora kiafya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 14 Agosti, 2018 nilipata fursa ya kwenda Namtumbo nikaenda kutazama kazi nzuri ambayo inafanywa na Wilaya ya Namtumbo. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kasi ambayo nilishuhudia kwa macho yangu na hasa baada tena kupeleka hizo shilingi milioni 500 naamini kazi ya kumalizia ujenzi haitachukua muda mrefu. *(Makofi)*

Naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, aendele kukiamini Chama cha Mapinduzi na Serikali yake kwasababu tumeahidi na tunatekeleza. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka

MHE. ZUBERI M. KUHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimsifu Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Wizara yote kwa ujumla kwa kutupatia fedha za kujenga vituo vya afya viwili ambavyo sasa viko kwenye asilimia 90 ya ujenzi wake, lakini Halmashauri ya Wilaya ya Liwale bado ina tatizo kubwa la kukosa hospitali yenye hadhi ya kuwa Hospitali ya Wilaya na wananchi kwa kuliona hilo wametenga eneo ambalo halihitaji hata fidia wananchi wamelitoa bure kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

Je, Serikali iko tayari kutusaidia kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Liwale?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata fursa ya kwenda kutembelea Wilaya ya Liwale na bahati nzuri nilikuwa na Mheshimiwa Mbunge na tukaenda Kituo cha Afya Kibutuka na ari ya wananchi wa Wilaya ile siyo ya kutilia mashaka. Naomba nimuondoe wasiwasi hizi hospitali 67 ambazo tunaanza nazo ni mwanzo tu, ni wajibu wetu kuhakikisha Wilaya zote Tanzania ambazo hazina Hospitali za Wilaya zinakwenda kujengewa. Naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, tukimaliza hospitali 67 tutaendelea kwenda katika Wilaya zingine ambazo bado hazina Hospitali za Wilaya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante wka kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwenye hii Wizara na swali hili ni muhimu sana.

Kama ambavyo iko Wilaya ya Namtumbo kuhusiana na suala la Hospitali ya Wilaya na hapa karibuni kwenye bajeti iliyopita, Serikali ilitenga shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Masasi pesa ambayo mpaka sasa

hivi haijankwenda. Hata hivyo nitaka kufahamu vigezo ambavyo vinatumika kati ya kuamua kujenga Hospitali ya Wilaya lakini na vituo vya afya ni umbali gani kutoka kimoja mpaka kingine kwa sababu kuna mvutano mkubwa sana uliopo Wilaya ya Masasi kwa sababu ya jambo hilo. Kati ya Kituo cha Afya na Hospitali ya Wilaya panatakiwa pawe na umbali gani? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hospitali 67 za Wilaya zote tayari Serikali ilishapeleka shilingi milioni 500; hakuna hata sehemu moja ambayo hatujapeleka. Ni vizuri Mheshimiwa Mbunge aka-*cross check* na kule anakotoka kama wanamwambia kwamba fedha haijafika naomba nimhakikishie fedha ishafika na nilipata fursa ya kwenda kwenye Jimbo lake bahati mbaya nadhani alikuwa na suala la kesi, lakini nilitamani tuwe naye ili tuweze kujionea na kutatua kero za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la kwamba ni umbali gani kati ya Hospitali ya Wilaya na Kituo cha Afya na mvutano ambao unatokea, naomba Mheshimiwa Mbunge yale ambayo yanatakiwa yatatuliwe na Halmashauri maana kuna vikao kule ambavyo ni vikao halali na sisi tunaviheshimu ni vizuri yale ambayo yanatakiwa yatatuliwe kule yakatatuliwe na ndiyo maana ya *D by D*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Justin Monko

MHE. JUSTIN M. MONKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Awali ya yote napenda sana niishukuru Serikali kwa fedha shilingi milioni 500 ambazo tumeshapata na sisi kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarafa ya Mtinko yenye Kata sita haina kituo cha afya hata kimoja na wannachi wka miaka mitano iliyopita wamekwishakujenga jengo ambalo limefikia katika hatua ya kupaua. Je, Serikali iko tayari sasa kuweka nguvu pale, kupeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha jengo hilo ili wananchi waweze kupata huduma ya afya?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, najua ni kiu ya Waheshimiwa Wabunge wangependa leo ikiwezekana Kata zote ziwe na vituo vya afya na naomba Mheshimiwa Mbunge akubaliane na kasi ambayo inafanywa na Serikali, tumeanza kujenga vituo vya afya tunakwenda kufikia 350 vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kasi hii naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira na hauko eneo ambalo ziko kata wamesema sita hakuna kituo cha afya katika awamu zinazofuata tutahakikisha maeneo yela ambayo hayana vituo vya afya vya jirani tutatilia mkazo twende huko, naamini na yeye itakuwa miongoni mwa wafaidika.

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala Mbunge wa Nkenge na linaulizwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Na. 108

Soko la Pamoja la Afrika Mashariki

MHE.BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA aliuliza:-

Je, ni nini mafanikio ya utekelezaji wa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa swali hilo namuona Dkt. Kijaji, Naibu Waziri, Wizara ya Fedha na Mipango hapo ndio penyewe.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, mwalimu wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruksa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilianzishwa rasmi mwaka 1999 kwa Wakuu wa Nchi za Jamhuri Uganda, Jamhuri ya Kenya na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusaini Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki mnamo tarehe 30 Novemba, 1999 na kuanza kutumika tarehe 7 Julai, 2000. Nchi za Burundi na Rwanda zilijiunga mwaka 2007 na Nchi ya Sudan Kusini ilijiunga mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 5(2) cha Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kimeanisha hatua nne za mtangamano ambazo ni umoja wa forodha, soko la pamoja, umoja wa fedha na hatimaye shirikisho la kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko la pamoja ni hatua ya pili ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo itifaki yake ilisainiwa mwezi Novemba, 2009 na kuanza utekelezaji wake mwezi Julai, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa soko la pamoja la Afrika Mashariki umewezesha watanzania na wananchi wa nchi wanachama kutembea kwa uhuru katika nchi za Jumuiya, kuongezeka kwa biashara ya bidhaa na huduma baina ya nchi wanachama na kupungua kwa idadi ya vikwazo vya kibiashara baina ya nchi wanachama kutoka 158 mwaka 2010 hadi kufikia 31 mwezi Julai, 2018. Aidha, kumekuwa na ongezeko la makampuni na wafanyabiashara kufungua shughuli za kuchumi katika soko la Jumuiya. Katika kipindi cha utekelezaji biashara baina ya nchi wanachama imeongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 3.4 mwaka 2009 hadi kufikia dola za Marekani bilioni 5.4 mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia 56.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa soko la mitaji Tanzania imefanikiwa kufanya marekebisho ya sheria za uwekezaji mitaji na kuruhusu Watanzania kushiriki katika soko la mitaji katika jumuiya. Katika kipindi cha mwaka 2013 hadi mwaka 2017 mtaji wa jumla wa soko katika Soko la Mitaji la Tanzania umeongezeka kutoka fedha za kitanzania trilioni 14.1 hadi kufikia trilioni 19.3 mwaka 2017. Aidha, Jumuiya ya Afrika Mashariki ipo katika hatua ya kuunganisha masoko yake ya mitaji kwa njia ya mtandao ili kurahisisha ununuzi na uuzaji wa hisa za makampuni mbalimbali katika soko la mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa nchi za jumuiya wameendelea kupata ajira katika soko la ajira katika maeneo yaliyofunguliwa. Katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2018 idadi ya Watanzania waliopata ajira imeongezeka hadi kufikia 566 ukilinganisha na Watanzania 364 katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2017. Aidha, haki ya ukaazi hutolewa kwa kila raia wa nchi za Jumuiya ya wanaokidhi vigezo vilivyoainishwa katika ibara ya 14 ya Itifaki ya soko la pamoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Balozi Kamala.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru kwa majibu yaliyotolewa lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa soko la pamoja hadi sasa ni wastani wa miaka nane toka tuanze kutekeleza na kwa kuwa Tanzania wakati tunajadiliana kuhusu kuanzisha Soko la Pamoja tulichelewa kuanza kufungua soko letu kwa baadhi ya maeneo tumekuwa tukifungua taratibu na sasa tumeshafungua karibu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua kama Tanzania kama nchi kama tumefanya tathmini ya kujua athari za kufungua maeneo yote na kama tathmini hiyo imefanyika nitafurahi kupata nakala ya tathmini hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwa kuwa inaonekana Watanzania waliopata ajira katika soko la Afrika Mashariki wameongezeka kutoka 364 hadi 566 kulingana na majibu idadi hii ambayo naona mimi nadhani ni ndogo ningependa kujua tu idadi hii ni jumla ya watanzania wote waliopata ajira katika soko la Afrika Mashariki kwa sababu kama ni jumla itakuwa ni kidogo sana au ni wale kwa hicho kipindi na tunajipangaje kuongeza idadi ya watanzania kuwa katika Afrika Mashariki? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa maswali hayo jibu maswali mawili tu Mheshimiwa Dkt. Kijaji.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tathmini ya athari ya kufungua maeneo yote kwa ajili ya Soko la Pamoja napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako tukufu Serikali yetu sasa hivi ndio inafanya tahmini ya

kufungua maeneo yote ili tuweze kujua na tutakapokamilisha kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge tutampa taarifa hiyo na Bunge lako tukufu litapata taarifa hiyo ya athari ya kufungua maeneo yote kwa ajili ya soko la pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira, hii ni jumla ya Watanzania ambao wako kwenye *formal employment* katika nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mheshimiwa Mbunge anauliza tumejipangaje kwa sababu idadi hii ni ndogo; naomba nimwambie kama Taifa tumejipanga kuendelea kuhakikisha tunaimarisha mifumo yetu ya kielimu ili Watanzania waweze kuwa *competitive* kwenye soko la Afrika Mashariki na waweze kupata ajira hizi kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe angalizo tu kwa watanzania wote hasa vijana wetu wanaotafuta ajira soko lipo kwa ajili yao na wao wachukue fursa hizi na wachukue *initiative*, pale zinapotangazwa nafasi hizi na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imekuwa ikitangaza mara kwa mara nafasi hizi, ni wakati sasa wa vijana wa Kitanzania waliopata elimu kwenda kuchukua ajira hizi. Lakini kwa sekta binafsi ni wakati sasa wa sekta binafsi kuchangamkia fursa hizi za zaidi ya wananchi wa Afrika Mashariki zaidi ya bilioni 185 ili tuweze kupeleka pia kuuza bidhaa zetu na kuzalisha ajira zote ambazo ni za moja kwa moja na ajira zile ambazo ni *indirect*. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Khatib.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Zanzibar inaingia Afrika Mashariki kupitia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wafanyabiashara wa Zanzibar wanatamani sana kufanya biashara na kufaidi soko la Afrika Mashariki, lakini kumekuwa na vikwazo vikubwa kwa bidhaa za Zanzibar kuingia Tanzania Bara ambalo ndio daraja kuu la kufikia Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri atupe muongozo kwa sababu Tanzania Bara

mmeweka vikwazo kwa bidhaa za Zanzibar kuingia hapa je, tutalifikiaje soko la Afrika Mashariki wakati daraja kuu la kufikisha bidhaa zetu mmetuwekea vikwazo? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango kwa niaba.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Khatib kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hakuna vikwazo vilivyowekwa na Tanzania Bara kuhusu bidhaa zinazozalishwa Zanzibar. Hilo naomba Watanzania walifahamu na ili kuthibitisha hili katika Watanzania wanaofaidi soko la Afrika Mashariki ni ndugu yetu mwekezaji mkubwa kutoka Zanzibar Bakhresa, anatoka Zanzibar na bidhaa zake ndizo zinazoongoza kuuzwa Tanzania na Afrika Mashariki. Kwa hiyo, niwathibitishie Watanzania Bara na ndugu zangu Wazanzibar wote hakuna vikwazo vyovyote vya wao kuja kuuza bidhaa zao Tanzania Bara na hatimaye kulifikia soko letu la Afrika Mashariki.

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa, tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amiri, Mbunge wa Viti Maalum na linaelekekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Na. 109

Ufugaji Wa Kuku Nchini

MHE. ZAINAB M. AMIRI aliuliza:-

Zipo aina mbili za ufugaji ambazo ni ufugaji wa kienyeji na ufugaji wa kisasa. Ufugaji wa kuku wa kisasa hutumia dawa nyingi sana katika ukuzaji na hutumia muda wa wiki tatu hadi nne kutumiwa na binadamu.

(a) Je, kuku hao wana madhara gani kwa binadamu?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia wafugaji wa kuku kutumia njia bora ya kisasa ambayo haina mashaka kwa watumiaji?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Ulega.

NAIBU WAZIRI MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amiri, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba ulaji wa nyama ya kuku wa kisasa au mayai ya kuku wa kisasa hauna madhara. Aidha, ufugaji wa kuku wa kisasa hauendani na matumizi ya dawa kwa wingi kama ilivyoainishwa kwenye maelezo ya swali la msingi. Vyakula vinavyotumika kwenye kulisha kuku wa kisasa huwa ni viini lische kama madini , vitamin, protini na nishati pamoja na chanjo ambazo sio dawa ambavyo ni muhimu kwa ukuaji na afya ya kuku na havina madhara kwa afya ya mlaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa haraka wa kuku wa kisasa unaofanya kuwa tayari kwa matumizi ndani ya kipindi kifupi cha wiki nne mpaka sita hutokana na ulishaji wa vyakula vyenye ubora pamoja na kuwepo kwa vinasaba vya ukuaji wa haraka nasio matumizi ya madawa au vichocheo pia hakuna uthibitisho wa kisayansi wa madawa au vichocheo kusababisha ukuaji wa haraka wa kuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji wa kuku kudhibiti vimelea vya magonjwa ili kupunguza matumizi ya madawa katika ufugaji wa kuku wa kisasa. Baadhi ya mikakati ni pamoja na kusajili na kusimamia mashamba ya kuku wazazi

na vituo vya kutotoleshea vifaranga ili kuzalisha vifaranga wasio na magonjwa. Kushirikiana na wadau kuendesha mafunzo kwa wafugaji juu ya ufugaji wa kuku unaozingatia usalama wa mazingira yaani *bio-security* na mbinu za ufugaji bora wa kuku. Aidha, Serikali inaendelea na mkakati wa kusimamia na kusajili utengenezaji wavyakula vya kuku vyenye ubora ili kupunguza usambazaji wa vyakula vyenye vimelea vya magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali inasimamia Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali ya Vyakula vya Wanyama Namba 13 ya mwaka 2010 na kanuni zake zinazotukataza matumizi ya madawa na vichocheo kwenye vyakula vya kuku ili kulinda afya ya mlaji. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Zainab.

MHE. ZAINAB M. AMIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu la msingi la Mheshimiwa Waziri amesema kuwa kuku hawa wa kisasa pamoja na mayai hawana madhara yoyote wa binadamu. Lakini kuna sintofahamu iliyojitokeza kwa baadhi ya wananchi kusema kwamba kuku hawa wana madhara mengi, baadhi ya madhara ni kwamba vijana wa kiume huota matiti na wanawake kuota ndevu.

Je, Serikali ina mkakati gani sasa ya kufanya utafiti wa kisayansi kujua ukweli huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili kinga ni bora kuliko tiba, mara kwa mara kunakuwa na mlipuko wa mafua ya ndege, je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kutafuta chanjo ya mafua ya ndege ili kuweza kuwasaidia wafugaji wetu wanaofuga kuku?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

NAIBU WAZIRI MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni juu ya utafiti kutokana na kinachohisiwa kuwa ni madhara yatokanayo na ulaji wa kuku wa kisasa na mayai ya kisasa. Naomba nichukue nafasi hii kuwaondoa hofu Watanzania wote na kurejea maneno niliyoyajibu katika swali la msingi ya kwamba hakuna madhara yanayothibitishwa kisayansi yanayotokana na ulaji wa kuku wa kisasa na mayai ya kisasa yanayokwenda kupelekea kuota maziwa kwa wanaume ama kutoa ndevu kwa wanawake. Pamoja na maelezo yangu hayo lakini nachukua rai ya Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amiri ya kwamba Serikali ijikite katika kufanya utafiti wa kujua aidha kama liko jambo la namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni chanjo ya mafua ya ndege. Mafua ya ndege hayana chanjo, rai yetu kama Serikali kwa wafugaji wote wa kisasa na wale wa asili ni kuzingatia kanuni bora za ufugaji ikiwa ni pamoja na ulinzi na usafi wa mazingira ya kufugia kuku wale, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante Dkt. Sware na Mheshimiwa Kabati.

MHE.DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kw akunipa nafasi na ningependa kupata ufafanuzi kutoka kwa Serikali maadam imekiri kwamba ufugaji hususani wa kuku wa kisasa hauna madhara sasa ningependa kujua mikakati ya Serikali ni ipi tuwe na *confidence* nao kwamba kuku hao wanaozalishwa na watu mbalimbali, je, ni salama kwa kiasi gani maana yake kila mtu anakuwa anajifugia je, mnakuwa na mfumo kwamba mnatoa *certificate* fulani ili tuwe tuna uhakika kwamba hao kuku wanaofugwa ni salama kwetu sisi? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi jamani muda wetu sio rafiki na tuna shughuli nyingi sana leo.

NAIBU WAZIRI MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali ni kuendelea kufuatilia kama

nilivyosema katika jibu la msingi kwamba sisi tutaendelea kufuatailia mahala wanapozalisha na mahala wanapototoleshea vifaranga vyetu na mahala wanapozalisha vyakula vya kuku. Naendelea kuwatoa hofu Watanzania ya kwamba ulaji wa kuku wa kisasa na mayai ya kisasa kisayansi hakuna uthibitisho kuwa na madhara.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa ufugaji wa kuku ni kati ya shughuli za kiuchumi ambazo zinasaidia sana kupunguza umaskini wa kipato kwa wananchi hususani akina mama. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuinua kina mama katika tasnia hii ya ufugaji wa kuku?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Ulega.

NAIBU WAZIRI MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wetu kama Serikali ni nini katika kuwasaidia wakina mama kujihusisha na shughuli hii ya ufugaji wa kuku ili kuwainua kiuchumi, tumekuwa na mkakati mzuri sana na mfano mzuri ni mama mmoja ambaye naweza kumtolea mfano katika Bunge hili Tukufu wa kampuni ya *AKM Brites*, mama mzalendo anayesambaza vifaranga vya kuku aina ya *croilla* nchi nzima kupitia majukwaa ya akina mama. Kwa hiyo, akina mama wote wanayo fursa hiyo na walioko tayari katika kujiunga kwenye vikundi vya akina mama vya ushirika tunaweza kuwasaidia kupata *access*/kupata njia ya kuweza kufanya shughuli hii ya ufugaji na kujiinulia kipato chao na kipato cha Taifa letu.

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

Na. 110

Kupeleka Umeme Katika Kata za Kigoma Kusini

MHE. HASNA S. K. MWILIMA aliuliza:-

Tunatambua juhudi za Serikali kuziwashia umeme kata tatu za Kandaga, Kazura Mimba na Uvinza, lakini umeme huo umeishia barabarani.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka umeme kwenye vijiji vyote vya kata hizo tatu pamoja na taasisi za Serikali kama vile shule, zahanati na vituo vya afya?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) imedhamiria kupeleka umeme katika vijiji vyote nchini ikiwa ni pamoja na vijiji vya Wilaya ya Uvinza. Kupitia *REA* Awamu ya Pili ya Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Serikali imefikisha umeme katika Kata za Kandaga, Kazura Mimba na Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Uvinza umeme umefika katika Vijiji vya Uvinza na Ruchugi pamoja na kufikisha umeme katika Kituo cha Afya Ruchugi, shule za msingi mbili, shule moja ya watoto wenye mahitaji maalum, kituo cha polisi na zahanati. Katika Kata ya Kandaga umeme umefikishwa katika Vijiji vya Mlela na Kalenge pamoja na shule mbili za Kalenge na Mlela. Katika Kata ya Kazura Mimba umeme umefikishwa katika vijiji vya Mwamila na Kazura Mimba pamoja na zahanati na shule ya msingi ya Kazura Mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vilivyobaki vya Kandaga, Nyanganga, Sambala, Kajeje, Mwakizega, Malagarasi, Kabeba, Kateti, Kiseki, Rulinga, Kanyangiri na Chakuru vitapatiwa umeme kupitia REA Awamu ya Tatu. Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini (REA III) mzunguko wa kwanza unaoendelea kutekelezwa na mkandarasi CCC – *Etern Consortium* utakaokamilika mwezi Juni 2019. Taasisi zinazotoa huduma za kijamii katika vijiji hivyo kama vile shule, vituo vya afya, visima vya maji na zahanati zitapatiwa umeme kupitia mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za mradi zinajumuisha ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 83, njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 60, ufungaji wa transfoma 30 pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 1,276. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 5 na milioni mia sita laki tano. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Hasna Mwilima.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali, ila ninaomba niulize maswali mawili ya yongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba mkandarasi ameshamaliza kazi yake ya ku-*survey* vijiji vyote ambavyo vinatakiwa viingie/vipate umeme REA Awamu ya Tatu, lakini Ukanda wa Ilagala mkandarasi alitakiwa afanye *survey* mpaka kwenye Kijiji cha Kirando na Kijiji cha Msiesi, lakini sambamba na hilo mkandarasi huyu alitakiwa pia aendelee mpaka Basanza.

Swali langu, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kigoma Kusini, je, ni lini sasa mkandarasi ataanza kazi rasmi ya kusimika nguzo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Tunatambua Kata ya Kalya iko karibu sana na Jimbo la Mwese na Meneja wa TANESCO Koa wa Katavi ndio anaye-

operate kwenye Kata ya Kalya ndani ya vijiji vyote sita. Je, ni lini sasa mkandarasi huyo anayeshughulika na masuala ya *survey* kwenye Jimbo la Mwese atakwenda Kalya kwa ajili ya ku-*survey* ndani ya vijiji vyote sita?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri kwa Mheshimiwa Mwilima, Mbunge wa Uvinza, lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Mwilima jinsi anavyofuatilia masuala ya nishati kwa Wananchi wa Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mkandarasi ameanza kidogo amechelewa katika Mkoa mzima wa Kigoma, lakini katika Jimbo la Uvinza kwa Mheshimiwa Mwilima ni kweli mkandarasi ameshaanza kazi katika maeneo ya Kandaga, Kazura Mimba pamoja na Uvinza, kadhalika ataendelea pia, kufanya *survey* na ameshakamilisha *survey* maeneo ya Nguruka, Sunuka pamoja na Songambebe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ameuliza ni kwa lini sasa wataanza kazi, mkandarasi ameshaanza kuleta vifaa, ameshaanza kupeleka nyaya. Ni matumaini yetu kuja kufika tarehe 5 Desemba wakandarasi watakuwa wameshaanza kazi kwenye Jimbo lake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili ambalo nazidi kumpongeza sana Mheshimiwa Mwilima ni kwamba, ni lini sasa maeneo ya Kerando pamoja na Msiesi yataanza kufanyiwa *survey* na kupelekewa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya Wananchi wake wa Uvinza kwa kazi nzuri anayofanya, mkandarasi ataanza kufanya *survey* katika Kata ya Kerando pamoja na Msiesi wiki ijayo, lakini pia atakapokuwa anafanya hivyo, bahati nzuri sana Jimbo la Uvinza litapata wakandarasi wawili, mkandarasi wa kwanza anatokea Katavi na wa pili akitokea Kigoma na katoka Kata

ya Kalya ambayo iko umbali wa kilometa takribani 30 kutoka Msiesi itapata wakandarasi wawili na kazi itafanyika.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Charles Mwijage. Mbunge wa Muleba Kaskazini. (*Makofi*)

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na ikupendeze kabla sijauliza swali hili dogo la nyongeza, niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru wewe kwa niaba ya Mheshimiwa Spika na uongozi wote wa Bunge kwa namna ambavyo tumekuwa tukishirikiana na mkiniongoza katika kutekeleza majukumu yangu. Kupitia kwako na Bunge lako tukufu napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna ambavyo walinipa majukumu na kuweza kunisimamia.

Mwisho nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na watumishi wa Mungu kwa namna ambavyo wamekuwa wakiniombea kwenye maisha yangu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali dogo la nyongeza, mazingira ya Kigoma Kusini kabisa ni kama yale mazingira ya Jimbo la Muleba Kaskazini, katika Mpango wa *REA* Awamu ya Pili mkandarasi alitandaza nyaya kwa kiwango cha *HT* katika Kata za Ibuga, Kata za Kagoma, Kata za Ngenge, lakini umeme haukuweza kuwafikia wananchi, wananchi wakabaki na mambo (*pegging*).

Ningependa kujua ni lini Mheshimiwa Waziri wananchi watawashia umeme, ili waweze kufaidi umeme wa *REA*?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli maeneo ya muleba Kaskazini na muleba Kusini kazi ya

mkandarasi wa awamu ya pili haikukamilika vizuri, lakini kwa kutambua umuhimu wa umeme katika maeneo hayo, maeneo mengi tumeyapeleka katika mradi huu unaoendelea wa *REA* Awamu ya Tatu, *round* ya kwanza. Na Mheshimiwa Mbunge tu nimpe taarifa Kata za Kagonga pamoja na maeneo aliyotaja ya Ngenge na mengine yako katika Mradi wa *REA* unaoendelea, kwa hiyo, atapelekewa umeme katika *round* hii inayoendelea hivi sasa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini.

Na. 111

Hitaji la Umeme – Maeneo ya Jimbo la Morogoro Mjini

MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD aliuliza:-

Maeneo mengi ya Jimbo la Morogoro Mjini hususan Kata za Mlimani, Bigwa, Lugala, Makunganya, Mkundi na Kilobe hayana umeme.

Je, ni lini Serikali itawapatia umeme wananchi wa maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) limetenga bilioni 7.7 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kusambaza umeme katika Mkoa wa Morogoro ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 2.8 zitatumika kukamilisha miradi 37 ya upanuzi wa njia za usambazaji umeme na kufikisha huduma ya umeme katika maeneo mengine yakiwemo maeneo ya Kata za

Mlimani, Bigwa, Lugala, Makunganya, Mkundi na Lukobe. Kazi za kupeleka umeme katika maeneo hayo itakamilika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019. Maeneo ya vijijini yanaendelea kupatiwa umeme kupitia mradi wa *REA* Awamu ya Tatu pamoja na *Densification* Awamu ya Pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Oktoba, 2018 *TANESCO* imekamilisha utekelezaji wa miradi 22 ya upanuzi wa njia ya usambazaji umeme katika Manispaa ya Morogoro. Hadi sasa jumla ya wateja wa awali 3,585 wameunganishiwa huduma ya umeme.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Abdul-Aziz swali la nyongeza.

MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, katika miradi 22 ya umeme katika Jimbo la Morogoro Mjini ambayo anasema imekamilika kuna mingine haijakamilika mpaka leo, zimewekwa nguzo tu, nyaya za umeme hazijapitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili ni kuwa lini mradi wa kusambaza umeme katika maeneo 37 katika Jimbo la Morogoro Mjini itakamilika?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Mgalu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge Abood kwa kazi nzuri anayoifanya ya kufuatilia miradi mbalimbali ya kinishati katika jimbo lake na atakuwa shahidi kipindi cha mwezi wa tatu na mwezi wa sita mwaka huu tulifanya ziara pamojanae katika Jimbo la Morogoro Mjini na kufanya zaidi ya mikutano sita ya hadhara katika maeneo ambayo amesainisha na baada ya mikutano ile *TANESCO* na ninapenda nichukue fursa hii kupongeza sana Shirika la

TANESCO Mkoa wa Morogoro na Meneja wake kwa kazi nzuri aliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndio maana baada ya ziara ile na hasa baada ya Mheshimiwa Mbunge kuwasilisha changamoto hizi maeneo haya ambayo tumeyataja, mfano maeneo ya Mkundi, Tungi, Mafisa, Bigwa Kisiwani, Lukobe na baadhi ya maeneo mengi kwa kweli yameanza kupata huduma ya umeme. Kwa hiyo, swali lake la nyongeza ameuliza sasa maeneo yale ambayo bado, ili kusambaza umeme naomba niliagize Shirika la Umeme TANESCO wafanye haraka katika maeneo haya ambayo Mheshimiwa Mbunge amesainisha, lakini kwa kiasi kikubwa kwa kweli, kazi nzuri imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali lake la pili, mimi naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa Morogoro hapa ni njiani tu na kama ambavyo utaratibu wetu wa kufanya ziara katika maeneo mbalimbali, baada ya Bunge hili mimi na yeye tutaongozana ili tupite katika yale maeneo machache ambayo yamesalia, lakini la mwisho kwamba katika Mkoa wa Morogoro pia mradi wa *Densification* Awamu ya Pili nao upo miongoni mwa mikoa 11 kwa kuwa Mkoa wa Morogoro nao unakua kwa kasi, hasa Manispaa ya Morogoro. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Nsanzugwako.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangazo la jana la Katibu Mkuu wa Hazina limetoa mwaka kwamba sasa Mkoa wa Kigoma unakwenda kuondokana kabisa na umeme mdogo kwa maana tutaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa na *African Development Bank* imetoa shilingi bilioni 400 kwa kujenga msongo mkuu kutoka Nyakanazi mpaka Kigoma.

Swali langu dogo nilitaka kumuuliza Waziri, kwa sababu njia hiyo ni ndefu kilometa 330, ni kwa nini sasa

wasione umuhimu wa kuwa na wakandarasi wawili mmoja akaanzia Nyakanazi kuja Kigoma na mwingine akaanzia Kigoma kuja Nyakanazi ili kazi iweze kukamilika kwa uharaka?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nishati,

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Nsanzugwanko kwa swali moja la nyongeza kwa niaba ya wananchi wa Kigoma, hongera sana Mheshimiwa Nsanzugwanko:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli. Kwanza niipongeze Serikali tumepata fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo na utekelezaji wa mradi huo unaanza mwezi Machi mwakani. Mradi huu ni mrefu na kimsingi unaanzia Iringa, Sumbawanga, Tunduma hadi Mpanda, lakini Kigoma hadi Nyakanazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli eneo hilo lina urefu wa takribani kilometa 322 na ni refu. Na kama alivyosema Mheshimiwa Nsanzugwanko sisi hilo tumeliona mapema na eneo hili litapata wakandarasi wawili wa ujenzi kwa ajili ya kuharakisha mradi huo.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Suleiman Nchambi.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa ruhusa ya swali dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza awali ya yote naomba nimshukuru sana Waziri wetu wa Nishati, ndugu yangu Mheshimiwa Kalemani na Naibu wake kwa kazi nzuri waliyoifanya katika Jimbo la Kishapu. Jimbo la Kishapu ni miongoni mwa majimbo ambayo yamepata umeme katika vijiji vingi sana katika awamu zote za *REA* na kwa kuwa vijiji vyote hivi zaidi ya 70 vimepata umeme, Mheshimiwa Waziri kuna Kituo cha Afya cha Bunambiu ambacho kina tatizo kubwa sana la umeme, kwanza naomba nikupongeze kwa kutupatia umeme vijiji vingi Wananchi wa Kishapu, lakini

nikuombe sasa utusaidie kituo hiki cha afya ambacho tumepata msaada wa *theatre* kutoka *Mkapa Foundation*, akinamama wanaweza kufanyiwa *operation* pale, tatizo letu kubwa ni umeme. Nikuombe ndugu yangu, najua umekuja zaidi ya mara tatu Kishapu, wewe na Naibu wako, nikuombe jambo hili dogo sana kwako katika Kituo chetu cha Afya cha Bunambiu. *Wabeja sana.*

MWENYEKITI: Ahsante, ni ombi.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Nchambi, Mbunge wa Kishapu, Mbunge *sharp* kwa kweli, kama alivyouliza swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli. Tumepeleka vijiji takribani 70 kwenye eneo lake na kati ya Wabunge ambao jimbo linaongoza sana kwa kutumia kifaa kinachoitwa *ohmmeter* ni pamoja na Jimbo la Kishapu. Amepeleka vifaa takribani 42 katika vituo vya afya na polisi, tunakupongeza sana Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kituo cha Afya cha Bunambiyu mkandarasi anaendelea kufanya *survey*. Ni matumaini yetu kuja kufika mwezi Machi au Aprili mwakani Hospitali na Kituo cha Afya cha Bunambiu kitapatwa umeme kupitia mradi wa *REA* unaoendelea hivisasa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge kuna wageni muhimu sana asubuhi hii ambao tunao kwenye Jukwaa la Spika, ambao ni wageni wa Mheshimiwa Spika. Ni wageni 19 wanatoka Jamhuri ya Watu wa China, nchi rafiki na Tanzania.

Tunao *His Excellence Cai Dafeng, Vice Chairman of the Standing Committee, the National People's Congress of the People of Republic of China.* Karibu sana. *(Makofi)*

Pia tunaye Bwana Hanibati, *Member of the Standing Committee of the Congress of the People's Republic of China,* karibuni sana. Tunaye Bwana Du Yubo, naye ni *Member of the Standing Committee of the NPC,* karibu. *(Makofi)*

Tunaye Bwana Weng Mengyong, *Member of the Standing Committee of NPC*. Pia tunaye pia Bwana Xia Huang, *Ambassador of the Department of African Affairs katika Ministry of Foreign Affairs of China*. Tunaye Bwana Liu Rui, *Deputy Director General of Foreign Affairs Bureau*. Tunaye Bwana Sun Wenpeng, *Deputy Director General of Liason Bureau*. (Makofi)

Pia tunaye Bwana Gao Xinyu, *Assistant Counsel of Bureau of Secretaries wa Chama cha NPC*. Tunaye Ms. Lan Mei, *Director of Foreign Affairs Bureau katika Chama Cha NPC*. Tuna Mr. Guo Yeling, *Deputy Foreign Affairs Bureau, General Office ya Standing Committee ya NPC*, karibu sana. Tuna Bwana Yan Lijun, *Associate Consultant kutoka General Office ya Standing Committee ya NPC* na tuna Yu Su, *Secretary wa His Excellence Cai Dafeng*. (Makofi)

Tunaye Bwana Wang Xiao, huyu ni mlinzi wa Mheshimiwa Cai Dafeng. Tunaye Huang Wei, *Third Secretary of the Department of African Affairs*. (Makofi)

Tunaye Wang Wei, *Third Secretary of the Department of African Affairs, Ministry of Foreign Affairs*. (Makofi)

Tunaye Wang Shuo, *staff wa Foreign Affairs Bureau ya Chama cha NPC*. (Makofi)

Tunaye pia, mkalimani kutika *Foreign Affairs*, Ms. Zhang Xin, karibu. (Makofi)

Tunao pia Ms. Wang Ke, Liang Lin, Dai Xu na Song Xing. (Makofi)

Karibuni sana katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. ninyi mnatoka kwenye nchi rafiki, ni urafiki wa damu na urafiki wa hali na mali, karibuni sana. (MAKofi)

Waheshimiwa tunaendelea.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Tunaendelea na maswali hawa wageni wetu wanaenda kuonana na Mheshimiwa Spika sasa hivi. Tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mbunge wa Ngara na linaelekezwa kwa Waziri wa Kilimo.

Na. 112

Kukamilika Mradi wa Ujenzi wa Soko la Mkakati Nzaza

MHE. ALEX R. GASHAZA aliuliza:-

Mradi wa Ujenzi wa Soko la Mkakati eneo la Nzaza Kata ya Kabanga mpakani mwa Tanzania na Burundi ulianza mwaka 2913 na ulitegemewa kukamilia mwaka 2014 kwa gharama ya shilingi 1,146,038,800/= lakini mpaka sasa mradi huo haujakamilika kutokana na Wizara ya Kilimo kutopeleka fedha. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha ujenzi wa Soko hilo?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Omary Mgumba.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mbunge wa Jimbo la Ngara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo ilitekeleza mradi wa kujenga masoko ya kimkakati likiwemo Soko la Nzaza katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, kupitia mradi wa uwekezaji katika kilimo Wilayani (*District Agricultural Sector Investment Project*) kuanzia mwaka 2006/2007 hadi 2014. Aidha, mradi huo uligharamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Soko tajwa ulitekelezwa chini ya Mkandarasi, Kampuni ya *Gross Investment Ltd* kwa usimamizi wa mtaalam elekezi Kampuni ya *Sky Architects*. Hata hivyo ujenzi wa soko hilo ulikabiliwa na baadhi ya changamoto ikiwemo uwezo mdogo wa mkandarasi na tatizo la upatikanaji wa fedha kwa wakati na hivyo kusababisha mradi kutokamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushughulikia changamoto hizo, Wizara itateua timu ya wataalam kwa ajili ya kufanya tathmini ya ujenzi wa masoko hayo ikiwemo Soko la Nzaza, kwa lengo la kushauri namna bora ya kukamilisha ujenzi wa masoko hayo na hatua za kuchukua kwa aliyehusika kukamisha ujenzi wa masoko hayo. Timu ya wataalam itakuwa na jukumu la kukagua kwa kina utekelezaji wa mikataba ya ujenzi wa masoko hayo, ubora wa kazi uliofanyika, uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha ujenzi wa masoko unakamilika, Serikali katika mwaka wa fedha 2018/2019 imetenga kiasi cha shilingi milioni 89 kwa ajili ya kutathimini hatua za ujenzi na mahitaji halisi ya gharama za ujenzi ili kukamilisha masoko yote ya kimkakati likiwemo soko la Nzaza ili kuhudumia wananchi katika Wilaya ya Ngara na kwingineko nchini.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Gashaza.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri; sasa naomba niulize maswali madogo ya nyongeza mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika jibu la msingi Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba changamoto zilizokumba mradi huu ni pamoja na uwezo mdogo wa mkandarasi huyu, na kwa kuwa mkandarasi huyu anadaiwa na wananchi walio-*supply* vifaa vya ujenzi kwake, walinzi wanaolinda *site* pamoja na baadhi ya mafundi zaidi ya milioni 20.

Je, Serikali itakuwa tayari kuwasaidia wananchi hawa kupata stahiki zao endapo mkandarasi huyo hataweza kuendelea na kazi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali namba mbili, kwa kuwa tunao mpaka pia wa Tanzania na Rwanda eneo la Rusumo na kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara imetenga eneo kwa ajili ya kujenga soko mkakati au soko la kimataifa katika eneo hilo; je, Serikali iko tayari kutenga fedha kwa ajili ya kujenga soko la kimataifa katika eneo hilo ambalo ni *strategic* kwa ajili ya kuinua kipato cha wananchi wa Jimbo la Ngara na Watanzania kwa ujumla?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo kwa kifupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)

: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii; napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza kama ifuatavyo:-

Swali lake la kwanza, kama alivyosema kwamba miongoni mwa changamoto zilizokabili mradi huu ni uwezo mdogo wa mkandarasi; na mkandarasi wakati anaondoka *site* kuna watu waliotoa huduma ambao waliingia mkataba na yeye kwamba wanam dai fedha. Anataka kujua kwamba Serikali tuna mkakati gani kuhusu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sisi kama Serikali tuliingia mkataba wa kutekelezewa huo mradi na mkandarasi, lakini mkandarasi naye aliingia mikataba ya kisheria na watoa huduma wengine, kwa hiyo kama Serikali tutahakikisha kwanza kama nilivyosema katika jibu la msingi, tunakwenda kuunda timu ya kitaalam kwenda kufanya tathmini ya kina ili kujua sababu zilizosababisha mpaka miradi hii kukwama, lakini pale itakapogundulika hatua za kisheria zitachukulia juu ya wote walihusika na hili na wale wote ambao kama huyu mkandarasi kuna watu wametoa huduma, tutahakikisha kwamba watu hao watalipwa kupitia

mikataba yao waliyoingia na huyo mkandarasi kwa mujibu wa sheria.

Swali la pili, ni kweli tunatambua hii miradi ilikuwa inatekelezwa katika wilaya tano mahususi kwa ajili ya masoko ya kimkakati katika mipaka yetu. Mimi binafsi nimhakikishie Mheshimiwa Gashaza, na nichukue nafasi hii kumpongeza sana katika kufuatilia hili, lakini nimwambie kama Serikali tunatambua mpaka huu wa Rusumo na fursa zilizopo, tuko tayari kwa ajili ya kuendeleza kwenda kujenga soko lingine la kimkakati katika mpaka huu na Rwanda kupitia *programme* ya kuendeleza sekta ya kilimo awamu ya pili maana yake *ASDP II*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Aida.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyanda za Juu Kusini tunazalisha mazao ya biashara na mazao ya chakula ambayo ni mazao mchanganyiko. Ningependa kujua kuwa Wizara ina mkakati gani wa kufungua soko, soko ambalo litakizi vigezo vya kibiashara, soko la kimkakati ambalo litasaidia ndani ya nchi yetu, lakini pia nje ya nchi ambazo ziko karibu na Nyanda za Juu Kusini?

MWENYEKITI: Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Omary Mgumba.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)
: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa niamba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Nyanda za Juu Kusini ni mikoa ambayo ni ya kimkakati na tunaitegemea sana katika uzalishaji wa mazao ya chakula katika taifa hili, ukizingatia kwamba zaidi ya asilimia 60 ya chakula cha nchi

hii inazalishwa katika Nyanda hizo. Kwa hiyo ni mipango ya Serikali kwanza kama sasa hivi tuna miradi ya kujenga maghala na maghala mengi tunajenga katika Nyanda hizo ambazo tulishaanza kujenga pale Makambaku, Rukwa, Katavi, Songwe na sehemu zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimhakikishie kwamba tunatambua fursa muhimu iliyokuwepo hasa katika Mkoa wa Rukwa na Katavi hasa ku-*access* soko la Congo. Tupo katika mikakati ya kujenga soko la kimkakati katika mpaka na congo ili tuondoke kwenye kujitegemea kuuza Congo kupitia soko la Zambia.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini linaelekezwa kwa Waziri wa maji.

Na. 113

Miradi ya Maji Mbulu

MHE. FLATEI G. MASSAY aliuliza:-

Miradi ya Maji iliyopo Mbulu Vijijini imekaa muda mrefu bila kumalizika mfano mradi wa ARR – Bashoy, mradi wa Tumatu, Mradi wa Bwawa la Dongobesh na mradi wa maji Haydom;

Je, Serikali haioni kuwa inawatesa wananchi wanaosubiri miradi hiyo bila mafanikio?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gregory Massay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa programme ya maendeleo ya sekta ya maji (*WSDP 1I*) Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ilipanga kutekeleza miradi ya maji 11, ambayo ni Haydom, Singu, Endamasak, Maretadu chini, Dongobesh, Arri-Harsha-Bashay, Moringa, Masieda, Endanyawish, Eshkesh na Mongahay-Tumati. Kati ya miradi hiyo, miradi ya maji sita (6) imekamilika katika Vijiji vya Singu, Endamasak, Maretadu chini, Dongobesh, Moringa na Masieda, na miradi ya maji mitatu (3) ya Haydom, Arri-Harsha-Bashay na Mongahay-Tumati inaendelea na utekelezaji. Miradi ya maji miwili (2) ya Endanyawish na Eshkesh imepanga kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2019/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi Haydom, Arri-Harsha-Bashay na Mongahay-Tumati upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2019 ambapo utekelezaji wa mradi wa maji Haydom umefikia asilimia 97 na unatoa huduma ya maji kwa wananchi. Mradi wa maji wa Arri-Harsha-Bashay umefikia asilimia 50 na Mongahay-Tumati umefikia asilimia 47 na utekelezaji wa miradi iliyobaki utafanyika katika awamu ya pili ya programme ya maendeleo ya sekta ya maji (*WSDP II*).

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Massay

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza nimshukuru amefika na ameiona miradi hii ambayo ameitaja yeye mwenyewe. Kwa kuwa miradi hii imefikia kwenye asilimia alizotaja yeye, na miradi hii haijakamilika na ni vigumu sasa kumtua mama ndoo kichwani.

Je, ana mkakati gani kama Serikali kumalizia miradi hiyo aliyoitaja yeye mwenyewe Mheshimiwa Naibu Waziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Vijiji vya Eshkesh, Enamilay, Labay, Maretadu, Gidim, Gorat, Maskaroda, Endanyawish, vimesaini mkataba na *DDCA* ya kuchimbiwa

visima. DDCA mpaka leo hawaonekani tangu Januari hadi sasa ninavyozungumza.

Je, ni lini sasa DDCA watakuja kuchimba visima hivi ili wananchi wa Jimbo la Mbulu vijijini wapate maji?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya kwa wananchi wake katika Jimbo la Mbulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini azma ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, ni kutua mwanamama ndoo kichwani na ukisoma Ilani ya Chama cha Mapinduzi inatutaka itakapofika 2020 tuwe na utekelezaji wa upatikanaji wa maji asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mjini. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Wizara ya Maji tumekwisha tekeleza miradi zaidi 1,595 ambayo imekamilika vijijini na imebakia miradi 4,92 ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Nataka nimuhakikishie kupitia Wizara ya Maji, chini ya Jemedari Mheshimiwa Mbarawa mkakati wetu ni kuhakikisha miradi 4,992 iliyobakia tunaikamilisha kwa wakati na Mheshimiwa Mbunge tunakulindia Ubunge wako kwa kukutekelezea miradi yako ya maji katika Jimbo lako la Mbulu.

Lakini kuhusu swali la pili, kuhusu suala zima la DDCA kwenye uchimbaji wa visima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wizara yetu ya maji tuna wakala wa uchimbaji visima yaani DDCA; labda niseme tu jukumu lao ni kuhakikisha wanachimba visima. Sasa sisi kama Wizara ya Maji tunawaagiza waende haraka Mbulu katika kuhakikisha vile visima ambavyo wamefanyia usanifu waweze kuvichimba na Mheshimiwa Mbunge wananchi wake waweze kupata maji safi na salama na yenye kuwatosheleza.

MWENYEKITI: Ahsante, nilimuona Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Dkt. Nagu.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapooonea hii miradi ya maji tuongee pamoja na *scheme* za umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *scheme* ya umwagiliaji ya Kata ya Ndungu ambayo imegharimu pesa nyingi sana za Wajapani sasa hivi ina hali mbaya sana, na si rahisi Mheshimiwa Waziri kuelewa bila ya yeye kufika.

Je, Mheshimiwa Waziri wa Umwagiliaji, huoni kuna umuhimu wa kwenda kuoia ile *scheme* ya maji ya Ndungu baada ya kumaliza Bunge hili? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, siko tayari kwenda kwa sababu sekta ya umwagiliaji imehamishiwa Wizara ya Kilimo, kwa hiyo nitaongea na watu wa Wizara ya Kilimo halafu wataweza kulifanya.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Nagu; Waziri? Haya Waziri tupate majibu hapa hapa.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli, yaani Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, imerudi Wizara ya Kilimo na ipo chini yangu mahususi kwa ajili ya kuingalia. Nakubaliana na ushauri

na ombi la Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge hili nitakuja Same kuja kutembelea mradi huo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na kwa dhiti kwa kunipa nafasi hii adimu na wananchi wa Kateshi wako hapo kwenye Gallery, naomba niulize swali dogo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru sana Serikali kwa kuweza kutupa na kututengea fedha kwa ajili ya maji ya Katesh ambao ni Mji Mkuu wa Hanang, ambapo kwa kweli maji ni kidogo sana na kama sasa kuna kina mama wanatoka mjini kwenda mbali kutafuta maji. Ninaomba kujua ni lini sasa mradi huu utakamilika ili akina mama ambao wanapaswa kuangalia watoto wao asubuhi wasiende mbali kutafuta maji? Nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge mama yangu Mary Nagu, ni mchapakazi mama jasiri katika kuwapigania wananchi wake wa Hanang. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Naibu Waziri wa Maji, nilipata rufusa ya Mheshimiwa Waziri kwenda katika Jimbo la Hanang katika kuangalia hali ya upatikanaji wa maji na utekelezaji wa miradi ya maji. Sasa sisi kama Wizara ya Maji tumeona haja sasa ya kuanzisha miradi mikubwa katika Jimbo la Hanang. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, azma ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha tunamtua mama ndoo kichwani. Kwa hiyo sisi kama Wizara ya Maji tutahakikisha miradi tuliyoanzisha Hanang inakamilika kwa mujibu wa mkataba na kuhakikisha inakamilika kwa wakati ili wananchi wako waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum na linaelekezwa kwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Na. 114

CAG kufanya Ukaguzi Maalum kwenye Miradi ya Maji

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA aliuliza:-

Kuna miradi ya maji ambayo imetekelezwa kwa gharama kubwa lakini baadhi haina ufanisi na miradi hiyo ikifanyiwa ukaguzi utawezesha kubaini ni fedha zilizotumika, miradi iliyokamilika na ambayo haijakamilika:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kumuagiza CAG kufanya ukaguzi maalum kwenye miradi hiyo?

MWENYEKITI: Jibu kwa swali hilo, Mheshimwa Naibu Waziri wa Maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimwa Conchesta, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amekuwa akifanya ukaguzi wa kila mwaka kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma (*The Public Audit Act, 2008*) ambapo hufanya aina mbalimbali za kaguzi kwa mujibu wa kifungu Na. 26 na 29 cha sheria hiyo. Ukaguzi wa miradi, ukaguzi wa ufanisi na ukaguzi wa kitaalam hufanyika kila mwaka ili kuhakikisha kuwa miradi ya maji inaendana na thamani ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa CAG ameshafanya ukaguzi wa ufanisi katika eneo la mikataba ya ujenzi wa miradi ya maji, udhibiti wa uchepushaji wa maji,

kutoka rasilimali za maji (*Control of Water Abstraction From Water Resources*) pamoja na ukaguzi wa usimamizi wa miradi ya uchimbaji wa visima vya maji (*Management of Boreholes Water Projects*) na usimamizi wa miradi ya maaji yaani (*Management of Water Projects*) kwa miradi iliyokamilika na inayoendelea. Taarifa ya ukaguzi huonesha fedha zilizotumika katika miradi ya maji ya hali halisi ya miradi (*status*) iliyokaguliwa na kuwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukaguzi wa kila mwaka unaofanywa na CAG pamoja na ukaguzi wa ufanisi (*Performance Audit*) na wa kitaalam (*Technical Audit*) ambao ni ukaguzi maalum wa miradi ya maji, Serikali haioni haja ya kumwagiza CAG kufanya ukaguzi mwingine maalum. Aidha, katika kuhakikisha kuwa miradi ya maji inatekelezwa kwa ufanisi, na gharama zenye uhalisia Wizara iliunda Tume maalum iliyohusisha wataalam wenye weledi kukagua namna miradi inavyotekelezwa hususani maeneo ya Vijijini.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Conchesta.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba tu niulize maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako malalamiko mengi sana kuhusu miradi ya maji, na mimi niko kwenye Kamati ya LAAC, tumekuwa tukikagua na kuangalia jinsi miradi hii inavyotekelezwa chini ya kiwango na ndiyo maana nilina kwamba kuna umuhimu wa CAG kukagua ili tuweze kujua na kubaini fedha kiasi gani zimetumika ni miradi mingapi imekamilika na ambayo hajakamilika.

Naomba niulize Serikali, ni kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi cha kuweza kukagua na kujibu haya mambo matatu niliyouliza hapa katika swali langu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Miradi hii inavyotekelezwa ni miradi ambayo Serikali inakopa na

Watanzania wanabeba mizigo mikubwa sana katika kulipa madeni hayo.

Je, Serikali haioni kwamba inaendelea kuwatwisha mizigo wananchi kwa kulipa madeni ya baadhi ya miradi ambayo haitekelezwi kwa ufanisi?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge, ni kweli kabisa moja ya miradi ya sehemu ambapo fedha za Serikali zilikuwa zikihujumiwa ni katika miradi ya maji; na ilifikia wakati watu walikuwa wakitaka kununua magari ya kifahari na kujenga maghorofa, walikuwa wakaja kuwekeza katika miradi ya maji. Hivyo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuona haja sasa ya wahandisi wa maji kuwaleta katika Wizara yetu ya maji. Lakini lingine ambalo nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kinga ni bora kuliko tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika Bunge lako Tukufu, sisi kama Wizara ya Maji tunawasilisha Muswada kwa mara ya kwanza kusomwa katika kuhakikisha tunaanzisha wakala wa maji vijijini. Hili litaenda kusaidia kusimamia miradi ya maji ili fedha za maji zisiwe zinafanyiwa ubadhilifu. Sisi kama Viongozi wa Wizara ya Maji, tumejipanga, na mpaka jana Mheshimwia Waziri ameshawafukuza zaidi ya wakandarasi wawili katika miradi ya Lindi pamoja na Kigoma, hii ni yote katika kuhakikisha tunasimamia miradi ya maji. Nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu hakuna mkandarasi yeyote wa maji atakaekula fedha za miradi ya maji na atakaekula fedha za miradi ya maji ajiandae kuzitapika mchana kweupe. ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, swali linalofuata linaulizwa kwa niaba ya Mbunge mwenye swali, linaulizwa na Mheshimiwa Leah Komanya; ni swali la Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguluka, Mbunge wa

Viti Maalum, linaulizwa kwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 115

Hitaji la Kivuko chenye Viwango – Kyanyabasa, Bukoba

MHE. LEAH J. KOMANYA (K.n.y. MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA) aliuliza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kivuko kilichopo Bukoba Vijijini Kyanyabasa hakikidhi viwango kabisa.

Je, ni lini Serikali itaweka Kivuko au Daraja litakalokidhi viwango?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguluka Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (*TEMESA*) inahudumia jumla ya vituo 20 vyenye vivuko 30 katika mikoa 12 ya Tanzania Bara, kikiwemo kivuko cha MV Kyanyabasa chenye uwezo wa kubeba tani saba (7), sawa na abiria 50 na magari madogo mawili (2). Kivuko hiki, kinatoa huduma kati ya Kasharu – Buganguzi katika mto ngono Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kivuko hiki kilifanyiwa ukarabati mkubwa mwezi Septemba, 2016 uliohusisha kufunga injili mpya. Kivuko kwa sasa kinaendelea kutoa huduma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa kivuko cha Kyanyabasa unakidhi mahitaji yaliyopo kwa sasa ya abiria na mizigo katika eneo hilo. Hivyo, Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (*TEMESA*) inaendelea kukihudumia kivuko hiki kwa kukifanyia matenezo ya mara kwa mara ili kuboresha utendaji kazi wake. Punde itakapobainika kuwa kivuko hakikidhi mahitaji Serikali itaangalia uwezekano wa kuweka kivuko kikubwa au kujenga daraja katika eneo hili.

MWENYEKITI: Asante, Mheshimiwa Leah Komanya.

MHE. LEAH J KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu ya Serikali kivuko hiki kimekuwa ni cha muda mrefu na kimechoka, gharama ya kujenga kivuko inakaribia na kujenga daraja, na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo Mheshimiwa Rweikiza amekuwa akikizungumzia mara kwa mara. Je sasa Serikali haioni haja ikawa na mkakati wa dharura wa kujenga daraja ili kuweza kuwaudumia wananchi wengi wakiwemo wa Kata Kishogo Kisharu, Nyakibibili na nyinginezo ili kuweza kuleta usafiri wenye ufanisi?

MWENYEKITI: Ahsante, Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leah Komanya, dada yangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa eneo hili kwamba baada ya matengenezo makubwa tuliyoyafanya kama tulivyojibu katika jibu la msingi kumekuwa na ufanisi mkubwa ni kwamba ile idadi ya safari za kuvuka katika eneo hili imeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimfahamishe tu Mheshimiwa bunge, hata kipato kwenye eneo lile kudhihirisha kwamba huduma imeongezeka kimeongezeka kwa asilimia

44. Pia kumekuwepo na tija kwenye matumizi ya kivuko kile, kwamba gharama zimeshuka kwa sababu ya matengenezo makubwa tuliyo yafanya. Nikuakikishie Mheshimiwa Mbunge pia kwamba, kama nilivyosema katika jibu la msingi, tunaendelea kuangalia, mahitaji yatakapokuwa yamefika sawia tutatengeneza daraja katika eneo hili ili kuweza kuwafanya wananchi waweze kupata huduma vizuri zaidi. Kwa hiyo tuvute subira wakati ukifika tutatengeneza daraja katika eneo hili.

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia Mbunge wa Chemba linaelekezwa kwa wizara hiyohiyo ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 116

Ukosefu wa Mawasiliano ya simu Lahoda

MHE. JUMA S. NKAMIA aliuliza:-

Kata ya Luhoda haina mawasiliano ya simu

Je, ni lini Serikali itajenga mnara wa mawasiliano ili kuondoka adha inayowakabili wananchi hao.

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Eng. Nditiye.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHANTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia Mbunge wa Chemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ilivianisha vijiji vya Kata ya Lahoda

ambayo awali vilikuwa miongoni mwa vijiji vya Kata ya Lalta kuwa vijiji vyenye shida ya huduma ya mawasiliano na kuingiza katika zabuni ya awamu ya kwanza iliyotekelezwa na Shirika la Mawasiliano (TTCL).

Mheshimiwa Mwenyekiti, TTCL ilijenga mnara na kuanza kutoa huduma kwa teknolojia ya *CDMA (Code Division Multiple Access)* baadaye kuhamia katika teknolojia ya *GSM (Global System for Mobile Communication)* mwezi Mei, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuhama kutoka teknolojia ya *CDMA* kwenda *GSM*, baadhi ya Vijiji katika Kata za Lahoda na Lalta vina shida ya upatikanaji wa huduma ya mawasiliano. Vijiji hivyo viliingizwa katika zabuni iliyotangazwa Juni, 2018 ya kufikisha huduma ya mawasiliano maeneo mbalimbali nchini na hatimaye kufunguliwa tarehe 20 Agosti, 2018. Hata hivyo, baada ya tathmini kukamilika Kata hizi hazikupata mzabuni. Hivyo Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote itavingiza vijiji vya Kata za Lohoda na Lalta katika zabuni zitakazotangazwa katika siku za usoni kutegemea na upatikanaji wa fedha.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Nkamia.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali, nilikuwa naomba niulize maswali mawili tu madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza Kata ya Lahoda pamoja na Kata jirani ya Ovada na Makorongo ni moja ya maeneo yana changamoto kubwa sana katika wilaya ya Chemba. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri aniakikishie, hizo siku za usoni lini zitakwisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nimetembea sana Tanzania kwa siku za karibuni, karibu robo ya nchi nzima, minara mingi ya mawasiliano ambayo imejingwa kwa fedha ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) imepambwa

na matangazo ya kampuni binafsi za simu. Hata pale Inyonga anapotoka Waziri wa Mawasiliano, Mheshimiwa Kamwele, mnara ule wa pale, hata pale Ipole, hata pale Katavi yote ina matangazo binafsi ya simu.

Je, Serikali inanufaika nini na matangazo haya ya makampuni binafsi ya simu?

MWENYEKITI: Ahsante, kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano Eng. Nditiye.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHANTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Juma Nkamia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Juma Nkamia kwa jinsi anavyofuatilia suala la upatikanaji wa huduma ya mawasiliano kwa wananchi wa jimbo la Chemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi suala la mawasiliano kwenye majimbo yao limekuwa suala la muhimu sana na hii inaonyesha jinsi Watanzania walivyotambua na kuhitaji kupata huduma ya mawasiliano. Sisi kama Serikali tumeendelea kufanya jitihada kwamba nchi nzima inapata mawasiliano ya kutosha kwa sababu mawasiliano ni uchumi na likini vilevile mawasiliano ni usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunatafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali kwa maeneo machache ya nchi yetu ambayo bado hayana mawasiliano na eneo la Lahoda likiwemo. Kwa hiyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Juma Nkamia kwamba pesa itakapopatikana, si muda mrefu kuanzia sasa hivi, tutafanya utekelezaji wa mradi wa mawasiliano kwenye eneo ambalo umeliomba. Naomba tu uwe mvumilivu tutafanya huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili, ni kweli Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imekuwa ikitekeleza ujenzi wa minara sehemu mbalimbali za nchi yetu na hasa zile sehemu ambazo hazina mvuto wa kibiashara kwa kushirikiana na baadhi ya makampuni ya simu. Ni kweli baada ya kutekeleza miradi mara nyingi zile kampuni za simu ambazo zinatumia hiyo minara huwa zinajimilikisha hiyo minara, lakini si sahihi. Minara hiyo inajengwa kwa nguvu za serikali kwa nguvu ya wananchi pamoja na hizo kampuni za simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nitoe maelezo na maelekezo kwa kampuni za simu, kwanza kabisa zitambue kwamba hile minara imejengwa kwa nguvu ya wananchi. Vile vile niwaelekeze Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kuanzia leo ninawapa siku 30; minara yote ambayo imejengwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwa kuunganishwa na nguvu na kampuni za simu ni lazima yawekewe mabango maalumu kuonyesha kwamba kuna nguvu ya Serikali. Tumewapa maelekezo hayo mwezi uliopita tulipofanya ziara na Kamati Kudumu ya Bunge ya Miundombinu lakini naona hawajatekeleza. Kwa hiyo Kuanzia leo tarehe 16 nawapa siku 30 minara yote ambayo imejengwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote waweke tangazo kuwaonyesha wananchi kwamba si minara inayomilikiwa na kampuni za simu.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Silvestry francis Koka Mbunge wa Kibaha Mjini linaulizwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Na. 117

Mkakati wa kutokomeza Ugonjwa wa Malaria

MHE. SILVESTRY F. KOKA atauliza:-

Lengo la Serikali ni kutokomeza ugonjwa wa malaria nchini;

Je, Serikali ina mkakati gani kukamilisha azma hiyo?

MWENYEKITI: Ahsante namuona Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa niaba, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

WAZIRI WA MALI ASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka Mbunge wa jimbo la Kibaha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano, inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli ina dhamira na nia ya kutokomeza magonjwa mbalimbali ikiwemo ugonjwa wa Malaria. Ili uhakikisha kuwa azma hiyo inafikiwa, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati muhimu ya kudhibiti malaria ambayo inayopendekezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO). Juhudi zinazofanyika katika kudhibiti Malaria, zimeleta maanikio kadhaa, ikiwemo kupungua kwa kiwango cha maambukizi ya malaria nchini kwa zaidi ya asilimia 50 kutoka asilimia 18.1 mwaka 2008 hadi asilimia 7.3 mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kufikia lengo la kupunguza zaidi maambukizi katika jamii, na hatimaye kutokomeza malaria nchini, Serikali kwa kushirikiana na wadau inatekeleza afua (*interventions*) mbalimbali za kinga na tiba ya malaria. Afua hizi pia zimetajwa katika Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ambazo ni pamoja na;

Kugawa vyandarua vyenye dawa (*Long Lasting insecticidal nets*) bila malipo, ili kuwakinga watu kuumwa na Mbu; kupulizia viuatilifu ukoko ndani ya nyumba (*Indoor Residual Spraying*); kuangamiza viluwiluwi wa mbu katika

mazalia (*Larviciding*); na kuhakikisha wenye dalili ya malaria wanapimwa ili kuthibitisha uwepo wa vimelea na matibabu sahihi kwa wale watakaothibitisha.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Koka.

MHE. SILVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nichukue fursa hii kuipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi chini ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi ya kupunguza kuenea kwa magonjwa haya ya malaria kutoka asilimia 18 hadi 7.3. Pamoja na hayo nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia bora ya kumaliza malaria ni kuzuia ugonjwa huu na hasa kumuamamiza mbu. Pale Kibaha kuna kiwanda pekee Barani Afrika kinachotengeneza viudadu, dawa ambayo haina madhara kwa binadamu wala kwa mazingira, unaweza hata ukainywa. Dawa hii inauwezo wa kushambulia viluilui vya mbu na kuviangamiza kabisa. Sasa swali. Serikali inatumia fedha nyingi kununua dawa kutibu malaria, kwa nini sasa sehemu ya fedha ya fedha hizo isipelekwe kununua dawa hizi na kuzipeleka hadi kwenye kaya na kuwaelimisha katika kampeni kabambe kama tulivyofanya katika vyandarua na kutokomeza malaria katika nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mnamo tarehe 22 Juni, 2017, Mheshimiwa Rais alitembelea kiwanda hiki ambacho kinauwezo wa kuzalisha dawa hizi lita milioni 6 kwa mwaka na aliagiza halmashauri za miji na majiji zinunue dawa hizi kwa ajili ya kuangamiza malaria, lakini hadi leo zoezi hili limeenda kwa kusua sua na sasa hivi kiwanda hiki kinaidai TAMISEMI takribani bilioni moja na milioni mia nne, hawajalipwa na hata wafanyakazi sasa wanakosa mishahara. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha fedha hizi zinalipwa ili kuendelea na azma kuendeleza viwanda vyetu vya ndani?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

WAZIRI WA MALI ASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kibaha Mjini Mheshimiwa Silvestry Francis Koka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa nini Serikali isiwekeze kwenye ununuzi wa *biolarvicides* ambazo zinatengenezwa pale Kibaha naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba agizo la Mheshimiwa Rais limetekelezwa kwa asilimia mia moja na takribani lita 250,000 ya hizo *biolarvicides* zinazotengenezwa pale kibaha zimenunuliwa na halmashauri zote za mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo utekelezaji wa agizo hilo unaendelea, na mwaka huu pia tumeweka kwenye bajeti za halmashauri zote nchini, mkakati wa kununua viudadu vinavyotengenezwa pale Kibaha. Serikali haiwezi kutumia mbinu hii moja tu kupambana na ugonjwa wa malaria, ndiyo maanda tunachanganya mikakati yetu, tuna mikakati hii ya kutumia *biolarvicides* ambazo zinatengenezwa hapa Tanzania pale Kibaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna mikakati mikoa ambayo ina maambukizi makubwa zaidi ya malaria kama vile Kigoma, Kagera, Geita, pamoja na Mara kwa ajili ya kufanya *indoor residual spray*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuna mikakati hiyo ya kugawa vyandarua kwa akina mama wajawazito wote wanapokwenda kliniki ambapo tumegawa vyandarua zaidi ya milioni sita katika kipindi cha mwaka mmoja, Kwa hivyo mkakati wetu ni *mixed, we have a mixed strategy* ya kupambana na ugonjwa wa malaria; ukichanganya na mkakati wa kutoa tiba baada ya mgonjwa kuwa amepimwa na kuthibitika ana vimelea vya ugonjwa wa malaria ni lazima atibiwe. Kwa hiyo atuwezi kutumia mbinu moja tu ya kutumia *biolarvicide* hata kama tunavitengeneza hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili nikwamba sisi kama nchi kuwa na kile kiwanda kwetu ni faida; na nina uhakika wawekezaji wa kiwanda kiwanda kile kwa kushirikiana na Serikali yetu hawakuwekeza kwenye mradi ule kwa ajili ya Tanzania peke yake, waliwekeza kwenye mradi ule kwa ajili ya kuuza kwenye nchi nyingine, ndiyo maana wanazalisha kiwango kikubwa kuliko ambavyo sisi kama Tanzania tungeweza kutumia kwa ajili ya matumizi ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza kuhusu fedha naomba nilichukue nitaliwasilisha kwa wahusika na Mheshimiwa Mbunge atajibiwa na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kadri ambavyo Serikali imejipanga.

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa kwa Wizara hiyo hiyo na Mheshimiwa Sikudhani Yassin Chikambo Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 118

Tatizo la Ukosefu wa Vifaa vya kujifungulia

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO aliuliza:-

Moja kati ya matatizo yanawakumba akina mama wajawazito ni ukosefu wa vifaa vya kujifungulia katika zahanati, vituo vya afya na hospitali;

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na tatizo hilo?

MWENYEKITI: Asante majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Kiwangalla.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Yasin Chikambo Mbunge wa Viti Maalumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto kwa sasa inatekeleza Mkakati wa Pili wa Kuboresha Afya ya Uzazi, Mtoto na Vijana wa mwaka 2016 hadi 2020 hapa nchini. Kati ya maeneo yaliyopewa kipaumbele katika mkakati huo ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kujifungulia na dawa muhimu za dharura za wakati wa ujauzito, uchungu, kujifungua na baada ya kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vifaa tiba na dawa muhimu kwa ajili ya huduma za afya ya uzazi na mtoto, viimegawanyika katika makundi matatu; wakati wa ujauzito, uchungu na kujifungua na baada ya kujifungua. Vifaa hivi kwa ujumla wake ni pamoja na dawa ya kuzuia na kutibu upungufu wa damu (*Fefol*), sindano ya kuzuia *Tetanus*, dawa ya kuzuia maambukizi ya Malaria (*SP*), sindano za antibiotiki (*Ampicilin, Gentamycin na flagyl*) dawa ya kuzuia kutokwa na damu nyingi (*oxytocin*), dawa ya sindano ya *magnesium Sulphate* kwa ajili ya kuzuia na kutibu kifafa cha mimba), kifungua kitovu cha mtoto, wembe wa kukatia kitovu, uzi wa kushona (*cut-gut*), mpira wa kulakia (*makin-tosh*) na mipira ya kuvaa mikononi (*surgical gloves*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vingine ni pamoja na kifaa cha kumsafisia mama ambaye ameharibikiwa na ujauzito, glovu ndefu za kuondolea kondo la nyuma lililokwama na vifaa vya muhimu kumsaidia mtoto kupumua anapozaliwa. Vifaa hivi vyote vinapatikana bure, bila, malipo katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali kubwa; hasa kufuatia ongezeko la bajeti ya dawa vifaa na vifaa tiba kutoka Bilioni 31 mwaka 2015/2016 hadi bilioni 270 mwaka 2018/2019.

Hasa kufuatia ongezeko la Bajeti ya dawa, vifaa na vifaa tiba kutoka shilingi bilioni 31 mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni 270 mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wito wangu kwa wananchi ni kuwaomba wajawazito wote wahudurie *Clinic* mara tu wanapogundua kuwa ni wajawazito na wajifungulie kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili waweze kupata tiba sahihi kutoka kwa wataalam wetu.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Sikudhani.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimimwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali na ufafanuzi uliotolewa, lakini zipo Hopitali na Vituo vya Afya ambavyo mpaka sasa wamekuwa wakiwaagiza akinamama wajawazito kwenda na vifaa vya kujifungulia ikiwemo hivi ambavyo wanasema vinatolewa bure:-

Je, Serikali inatoa tamko gani kwa Hospital na Vituo vya Afya ambavyo mpaka sasa wanashindwa kutekeleza maagizo ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwa niaba.

WAZIRI WA MALIASILI (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Serikali imeongeza bajeti ya dawa kutoka shilingi bilioni 31 zilizokuwepo mwaka 2015/2016 mpaka takribani shilingi bilioni 270 mwaka 2018/2019 na tunajitahidi kupeleka fedha kwenye vituo vyote, lakini pia kwa kuwa tumeimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya, sitarajii na ninarudia tena Mheshimiwa Chikambo, niangalie vizuri na *read my lips*, sitarajii kwamba bado mpaka sasa tunavyozungumza kuna Hospitali ama

Zahanati ama Kituo cha Afya kinachowadai akina mama wapeleke vifaa wakati Serikali imetenga bajeti ya vifaa na kwamba vifaa hivi vinatolewa bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi namwomba anipe orodha ya vituo hivyo ili niweze kufanya ufuatiji na hatimaye kuchukua hatua stahiki kwa Watendaji ambao bado wanatumia hila za kuwalaghai akina mama ili kujenga mazingira ya kupata rushwa na hatimaye kusababisha vifo vya akina mama wajawazito na watoto kuongezeka hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia, ni marufuku kwa Watendaji wa Kituo chochote kile cha Afya, Zahanati kudai akina mama wapeleke vifaa hivi kwa kuwa kwa sasa vinapatikana bure katika vituo vyetu vyote vya kutolea huduma za afya nchini.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, bado tupo Wizara hiyo hiyo. Swali linalofuatwa linaulizwa na Mheshimiwa na Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 119

Mapungufu ya Kimiundombinu Hospitali ya Mkoa wa Singida

MHE. JESCA D. KISHOA aliuliza:-

Hospitali ya Mkoa wa Singida ina upungufu sana wa miundombinu ikiwemo kukosekana kwa gari la wagonjwa (*Ambulance*), uhaba wa Watumshi na vifaa tiba anuwai.

Je, ni lini Serikali itatatua kero zinazowakabili wananchi wa Singida wanaotumia Hospitali ya Rufaa?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Afya, ipo katika hatua mbalimbali ya kuboresha na kuimarisha huduma za afya kwa wananchi wake katika Mkoa wa Singida. Hospitali ya Mkoa wa Singida imekuwa ikikabiliwa na tatizo la ukosefu la gari la kubebea wagonjwa (*Ambulance*) baada ya gari lililokuwepo kupata ajali mwaka 2016. Kwa kuona umuhimu wa gari hilo, katika Bajeti ya mwaka 2018/2019 hospitali imetengewa kununua magari mawili ya kubebea wagonjwa.

Mheshimwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu mingine, hospitali inaendelea kuimarika kwa kupitia Mpango Kabambe wa Uendeshaji wa Huduma za Afya (*Comprehensive Hospital Operational Plan*) ambao umejikita katika ununuzi na ukarabati wa vifaa tiba ili kukidhi mahitaji ya wananchi wa Mkoa wa Singida wanoutumia huduma ya afya katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Pia kupitia utekelezaji wa mradi huo, Hospitali imekamilisha jengo la kutolea vipimo vya mionzi kama vile *CT Scan* na *MRI*.

Mheshimwa Mwenyekiti, aidha, katika bajeti ya mwaka 2018/2019 Hospitali ya Mkoa wa Singida ilitengewe kaisi cha shilingi 160,000,000/= kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu yake. Fedha hizo zimeshawaliwa katika mkoa na ukarabati unaendelea na upo katika hatua za mwisho ambapo muda wowote Mkandarasi atakabidhi majengo yaliyokarabatiwa.

Mheshimwa Mwenyekiti, kwa upande wa Watumishi, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Hospital imepelekewa watumishi wapya wa kada tofauti za afya 54 na hivyo kupunguza uhaba uliokuwepo kutoka asilimia 54 mwaka 2017 mpaka kufikia asilimia 44 kwa sasa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jesca Kishoa.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetenga shilingi milioni 400 mpaka shilingi milioni 500 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi wa Vituo vya Afya nchini, lakini katika fedha hizo, Serikali haijatenga hata senti tano kwa ajili ya usimamizi wa kutekeleza miradi hiyo: Sasa Serikali haoni haja ya kutenga fedha hizo ili miradi hiyo iweze kutekelezeka kwa ufanisi mkubwa?

Swali la pili; Serikali imehamisha ma-*engineer* kutoka ngazi ya Halmashauri na kuwapeleka *TARURA* na Halmashauri zetu zimekuwa zikishindwa kutekeleza miradi mbalimbali kwa sababu ya ukosefu wa ma-*engineer* katika ngazi ya Halmashauri, sasa ni lini Serikali itaajiri ma-*engineer* wapya kwenye Halmashauri zetu ili miradi yetu ya maendeleo iweze kutekelezeka kwa wakati?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwa niaba.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii. Serikali inapeleka fedha kwa ajili ya Vituo vya Afya kila kona ya nchi yetu lakini hakuna fedha za usimamazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya fedha za usimamizi, fedha za utafiti, *feasibility study*, *consultant* ndiyo mambo ambayo Rais wa Awamu ya Tano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati wa kufungua Bunge hili aliyapiga marufuku. Mheshimiwa Rais hapendi kusikia mambo ya mchakakato unaendelea, tunajipanga, tunajijweka sawa; hataki kusikia habari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tulipokuwa tunaweka mikakati ya kunyanyua hadhi ya Vituo vya Afya nchini ili viweze kutoa huduma za upasuaji, viweze kutoa huduma za dharura. Namshukuru Mungu mkakati huu ulinisaidi kuokoa maisha yangu pale Kituo cha Afya Magugu, maana kama kingekuwa hakijapandishwa hadhi pengine

nisingepata *oxygen* na pengine nisingeweza ku-*survive*.
(*Makofi*)

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa hiyo, mkakati wetu huu wa kupandisha ubora wa huduma za afya zinazotolewa katika ngazi ya kati ya Kituo cha Afya umefanikiwa sana kwa sababu tumeondoa mambo ya michakato, tumeondoa mambo ya *consultancy*, tumeondoa mambo ya *monitoring and evaluation*, tumeondoa yote hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapeleka pesa, tunapeleka maelekezo na Mheshimiwa Jafo ni mkali kweli kweli katika usimamizi. Anachokifanya ni kuhakikisha Halmashauri kwa kutumia *resources* walizonazo, kutumia watu wao, kutumia mafundi wao (*local*), wanaendesha mchakato huo haraka na wanajenga vituo hivi. Nami sijaona kituo hata kimoja chenye upungufu. Kwa hiyo, tunaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine hii *business as usual* ya mambo ya usimamizi na mambo ya *monitoring* pengine tuitazame sana, pengine haina tija na inachuka tu gharama za Serikali nyingi na muda mrefu kama tunavyopata shida kwenye miradi ya maji na ndiyo maana sasa wanajipanga upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira kwa ma-*engineer*, kila mwaka Serikali inaweka bajeti na inaleta mapendekezo hapa Bungeni, Bunge linatupitishia Bajeti kwa ajili ya kuongeza watumishi. Kwa hiyo, idadi ya ma-*engineer* ambao wataajiriwa na kupelekwa kwenye Halmashauri, itaongezeka kadri sisi Bunge tunapitisha bajeti za ajira hapa Bungeni.

MWENYEKITI. Ahsante. Tunaendelea na swali letu la mwisho, leo linaulizwa na Mheshimiwa Anna Joram Gidarya, Mbunge wa Viti Maalum na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda Biashara na Uwekezaji

Na. 120

Ujenzi wa Kiwanda cha Chumvi Hanangi - Hanyara

MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y. MHE. ANNA J. GIDARYA) aliuliza:-

Wilaya ya Hanang' iliyopo Mkoa wa Manyara katika Kijiji cha Gendabi kuna Ziwa la Chumvi lililozalisha chumvi inayotumika kusindika ngozi. Mpaka sasa wanaofaidika na chumvi hiyo ni watu wachache wanaosafirisha kwenda nchini Burundi kwa ajili ya kusindika ngozi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutuma wataalam wa viwango na wa kuhakiki matumizi ya chumvi hiyo ili kujenga kiwanda bora kwa ajili ya kusindika ili kupata soko bora na vijana wengi kupata ajira ya kudumu kutokana na kiwanda hicho?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Joseph Kakunda.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Joram Gidarya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, chumvi ni muunganiko wa kikemikali wa madini ya *Sodium* na *Chloride* na sehemu kubwa inapatikana katika maji ya bahari na maziwa. Chumvi ina matumizi mengi ikiwepo kutumika katika chakula, usindikaji na uzalishaji wa aina mbalimbali za bidhaa, ikiwemo usindikaji wa ngozi.

Kwa kutambua umuhimu wa malighafi hiyo, mwaka 2012 Serikali kupitia wataalam wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilifanya utafiti ili kuangalia uwezekano wa chumvi

inayopatikana katika Ziwa Gendabi itumike kwa manufaa mapana zaidi na kutoa ajira kwa wananchi wa eneo hilo na Taifa kwa ujumla. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa itahitajika teknolojia ya kisasa itakayohakikisha kuwa chumvi inayozalishwa ni salama kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya matokeo ya utafiti huo, Serikali ilianza kufatuta mwekezaji mwenye uwezo wa kujenga kiwanda kitakachotumia teknolojia sahihi ya kuchakata madini hayo na hadi sasa bado hajapatikana mwekezaji wa uhakika. Kwa kuwa taarifa niliyoitaja hapo juu ni ya muda mrefu, namwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji atume timu ya wataalam mchanganyiko kutoka Wizarani, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *TIRDO* na *TBS* wakafanye uchunguzi kwa mara nyingine ili tupate uhalisia wa sasa. Taarifa yao ndiyo itaishauri Serikari vizuri zaidi kuhusu hatua zitakazofuata.

MWENYEKITI: Ahsante. Maswali ya nyongeza Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nataka kwanza nimweleze Mheshimwa Waziri kwamba jibu alilolileta hapa ni kutokana majibu yale ya *sound* yaliyokuwa yanatolewa na viongozi waliopita kwenye hiyo Wizara na ndiyo maana utaona kwenye hitimisho la jibu lake wanasema kwamba Serikali ilianza kumtafuata mwekezaji, lakini ukiendelea mbele wanaongelea habari ya kwamba wanataka warudie tena kufanya utafiti.

Sasa nataka awaeleze wananchi wa Kijiji cha Gendabi kama chumvi hii inasafirishwa kupelekwa Burundi sasa hivi na kwamba wanaongelea habari za kutafuta mwekezaji na pia wanasema wanataka warudie kufanya utafiti: Je, msimamo wa Serikali sasa hivi nini kuendelea na utafiti au kutafuta mwekezaji?

Swali la pili; suala hili la chumvi kwa sehemu kubwa sana pia linafanyika maeneo ya Pwani. Ukienda Pwani ya

Lindi na Pwani ya Mtwara pia pale kuna mashamba makubwa ya chumvi. Usumbufu wanaoupata wananchi wa Gendabi kuhusiana na masuala haya chumvi ni sawa sawa kabisa na usumbufu wanaoupata watu wa Mtwara na Lindi hasa maeneo ya Lindi, Machole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kufahamu kutoka kwa Serikali, haioni kwamba inatakiwa ifanye juhudi za makusudi kabisa ili kuwaondolea adha wale wakulima wa chumvi; kwa sababu mpaka sasa hivi kiropa kimoja cha chumvi cha kilo 50 kinauzwa shilingi 10,000/=; kwa nini tusiwatafutie masoko?

MWENYEKITI: Ahsante. majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Kakunda.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mwambe kwamba hakuna *sound* kwenye majibu ya Serikali. Nami nataka nimhakikishie kwamba ile *sound* ilikuwa ni ufafanuzi wa kina wa mambo ambayo yanajulikana kutokana na utafiti mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza, msingi ulikuwa ni kwamba kwanini kusijengwe kiwanda pale, badala ya ile malighafi kutoka pale kupelekwa Burundi? Huo ndiyo ulikuwa msingi wa swali. Tumejibu kwamba ule utafiti ulifanyika ulishauri teknolojia ya kisasa. Sasa kwa sababu teknolojia ya kisasa haijapatikana ile iliyoshauriwa, ndiyo maana nimemwagiza Katibu Mkuu atume timu nyingine kwenda kuangalia vizuri zaidi na kushauri katika teknolojia zinazotumika sasa hivi katika maeneo ya Uvinza na maeneo mengine ambayo yeye mwenyewe kayataja ili tuone kama tunaweza tukaitumia na kule Gendabi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna shughuli nyingi za uzalishaji wa chumvi zinafanyika katika mwambao wa bahari ikiwemo Lindi na maeneo mengine kama Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masoko, naomba nichukue changamoto aliyoitoa kama ushauri wa kuagiza wataalamu wetu kuangalia masoko ya ndani na nje ili tuangalie sehemu ambayo tunaweza tukapata bei zaidi tukaongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, wageni tulionao, kundi la kwanza nilitangaza kwa sababu ya umuhimu na shughuli walizonazo kwa leo.

Kundi la pili ni wageni watano wa Katibu wa Bunge kutoka Ofisi Msajili wa Vyama vya Siasa nchini ambao ni Ndugu Mohamed Ally Ahmed, Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, wameongozana Sist Nyahoza, Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa. Pia yupo Pinsia Kiure, Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa; na Ndugu Esther Mwanari, Mwanasheria Mwandamizi Ofisi ya Msajili wa vya Vyama Siasa.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Mbunge na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, ambao ni Ndugu Samwel Malugu, Mbunifu wa Shindano la Urembo la Dunia la *Miss Journalism World 2018*; Ndugu Godson Kirita, Katibu wa Kamati ya Maandalizi; na pia yupo Ndugu Shadow Islam, Mjumbe wa Kamati ya Maandalizi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 16 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde, Mbunge na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Vijana Kazi na Ajira ambao ni Wawakilishi wa *Tigo Fiesta Team* kutoka Jijini Dar es Salaam.

Timu hii kwa pamoja wamekuja Dodoma kwa ajili ya Tamasha lao la Tigo Fiesta litakaofanyika siku ya Jumapili tarehe 18 Novemba, mwaka 2018 katika Jiji la Dodoma likiwa na vipengele viwili ambapo ni kugeuza changamoto kuwa fursa na kutafuta Msanii wa Dodoma, yaani *super* nyota. Karibu sana wasanii wetu. *(Makofi)*

Tuna wageni 57 wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mbunge na Naibu Waziri wa Madini ambao ni Viongozi CCM wa Kata 19 za Jimbo la Maswa Mashariki, Wenyeviti, Makatibu, Makatibu Wenezi wa Kata wakiongozwa na Katibu wa CCM wa Wilaya hiyo, Ndugu Noverity Kibajaji. Karibu sana ndugu zetu. Mnamwona Mheshimiwa Nyongo yupo anachapa kazi mliyomtuma. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Waheshimiwa wa Wabunge wa CCM Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa kutoka Wilaya ya Kaskazini 'A', Mkoa wa Kaskazi ni Unguja wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM, Ndugu Ali Mkame. Ahsanteni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Vile vile tunao wageni sita wa Mheshimiwa Allan Kiula, Mbunge, ambao ni Viongozi wa CCM Kutoka Mkaoni Singida, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Kata, Ndugu Andrea Barnaba. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Haji Ameir Haji Ntimbe, Mbunge ambao ni ndugu zake pamoja na wapiga kura wake kutoka Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja wakiongozwa na mke wake Ndugu Kanima Khatib Haji. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni 17 wa Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua, Mbunge, ambao ni vijana wanatoa elimu kwa watu wenye hatari ya kupta virusi vya UKIMWI kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania wakiongozwa na Ndugu Halima Tina. Wako wapi? Karibuni sana.

Tunao wageni watatu wa Mheshimwa Charles Kitwanga, Mbunge, ambao ni wafanyabiashara kutoka Jimbo la Misungwi. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge ambao ni wadau wa maendeleo na watoto wake kutoka Nairobi, Kenya wakiongozwa na Ndg. Okemwa Omare. Ahsanteni sana, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 25 wa Mheshimiwa Mary Nagu Mbunge, ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake Hanang, wakiongozwa na Ndugu Paschal Ero. Karibuni sana wageni wetu. Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Jumaa Aweso Mbunge, Naibu Waziri wa Maji ambao ni wapiga kura wake kutoka Pangani, Mkoani Tanga Ndugu Waziri Mbezi na Ndg. Samba Mwinyihaji, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge ambao ni mpigakura wake kutoka Jimbo la Mlalo Ndugu Khalifa Kimomwe. Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Ally Ungando, Mbunge, ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake Kibiti, wakiongozwa na Ndugu Leonald Felix. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa ambao ni wanafunzi kutoka *St. John University* ya Jijini Dodoma, Ndugu Elizabeth Kayombo na Ndugu Vanidicta Kalinga. Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Venance Mwamoto Mbunge ambaye ni Rais Mstaafu wa Mazingira Afrika Dkt. Terezya Luoga, huyu aliwahi kuwa Waziri wetu wa Nchi, karibu sana Mheshimiwa Terezya, bado tunakukumbuka. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge ambao ni kwaya ya akina mama wa Anglikana kutoka Mkoani Iringa, wakiongozwa na Ndugu Rehema Mwalongo, wamependeza kwelikweli, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge ambao ni Mwalimu Sulgasa Naman, mwalimu wake wa shule ya msingi na Ndugu Clara Ombay kutoka Mbulu Vijijini, hongera. *(Makofi)*

Tuna kundi la tatu la wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 60 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Tawi la Dodoma, karibuni sana mmekuja kwa mafunzo. *(Makofi)*

Wageni watatu ambao ni wachungaji kutoka Kanisa la *Tanzania Assemblies of God (TAG)* kutoka Moshi, Mkoani

Kilimanjaro wakiongozwa na Mchungaji Isaya Temu, karibuni sana kwa mafunzo. (*Makofi*)

Tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa William Ngeleja kuhusu mashindano ya Mabunge ya Afrika Mashariki.

Kwa niaba ya Kamati Tendaji ya wachezaji wote wa *Bunge Sports Club* kwa ujumla anaomba kuwasilisha shukrani zetu za dhati kabisa, wao ndio wanamshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Waziri Mkuu kwa niaba ya Serikali na Katibu wa Bunge kwa utayari wa kuiwezesha *Bunge Sports Club* kushiriki mashindano ya michezo ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yatakayofanyika Jijini Bujumbura, Burundi kuanzia tarehe 30 Novemba 2018 hadi tarehe 10 Desemba 2018.

Katika mashindano haya msafara wa *Bunge Sports Club* unawakilishwa na wachezaji 60 pamoja na Sekretarieti ya watu 10. Kutokana na hamasa kubwa ya Waheshimiwa Wabunge na watumishi wengi kushiriki katika mazoezi ilikuwa mtihani mkubwa kwa makocha na Kamati Tendaji kuteua wawakilishi katika mashindano hayo miongoni mwa wanamichezo zaidi ya 160 kupata hiyo idadi ya wachezaji 60 waliosheheni vipaji mbalimbali wanaohudhuria mazoezi kila siku viwanjani.

Kamati Tendaji inauomba uongozi wa Bunge na Serikali pamoja na Bunge kwa ujumla tuendelee kuboresha bajeti ya michezo ili kuwezesha kukidhi mahitaji ya wachezaji kwa kila mchezo, hili ndio ombi la msingi.

Aidha, wachezaji wote walioteuliwa wanaombwa kuhudhuria kikao cha wachezaji kitakachofanyika kesho tarehe 17 Novemba, 2018 katika Ukumbi wa Msekwa saa 5.00 asubuhi baada ya mazoezi.

Mheshimiwa Jenista, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anapenda niwatangaze wageni wawili ambao ni ma-*sister* kutoka Chipole, karibuni sana ma-*sister*. Endeleeni

kutuombea taifa hili na tunathamini sana kazi mnayoifanya.
(Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndio matangazo yalikuwa mbele yangu na kwa sababu ya shughuli Waheshimiwa Wabunge angalieni *Order Paper* imesheheni mambo mengi sana leo na kutokana na hilo nilikuwa nawasihi sana sitakubali kuchukua mwongozo.

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:

KAULI ZA MAWAZIRI

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (*JICA*) litaendesha mashindano ya pili ya riadha kwa wanawake kutoka mikoa yote nchini katika Uwanja wa Taifa - Dar es Salaam tarehe 24 na 25 Novemba, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la mashindano haya ya riadha ni kuibua vipaji katika riadha vilivyofichika upande wa wanawake, vipaji ambavyo Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa michezo itavilea ili ifikie viwango vya kimataifa na kuweza kuiwakilisha nchi kwenye mashindano makubwa ya kimataifa yajayo kama mashindano ya *All Africa Games* yatakayofanyika Casablanca, Morocco mwakani na mashindano ya *Olympic* yatakayofanyika nchini Japan mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyokuwa kwa mashindano haya mwaka jana, watoto wa kike wanaofanya vizuri wanapewa fursa ya kushiriki kwenye mashindano mbalimbali ya riadha ya kimataifa yakiwemo ya Mbio Ndefu ya Naghai, Japan yanayofanyika kila mwaka. Washindi wetu wa mwaka jana wasichana wawili kutoka Arusha na mmoja kutoka Ukerewe, Mwanza waliwakilisha nchi kwenye

mashindano ya marathoni ya Naghai, Japan mwezi Oktoba mwaka huu na wote watatu walirejea nchini na medali. Silvia Masani kutoka Ukerewe, Mwanza alipata medali ya shaba, Rozalia Fabian kutoka Arusha alipata medali ya fedha na Amina Mohamed vilevile kutoka Arusha alipata medali ya dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa ya Arusha na Mwanza na wakuu wao wa Wilaya na vilevile Waheshimiwa Wabunge wote wa mikoa hiyo kwa malezi na maandalizi mazuri ya vijana wao hadi kuanza kufanikiwa kimataifa katika riadha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii vilevile kuwahimiza Waheshimiwa Wabunge wote kuhakikisha kuwa mikoa yao inashiriki kikamilifu kwenye mashindano ya riadha ya watoto wa kike tarehe 24 na 25 mwezi huu wa Novemba Jijini Dar es salaam. Mpaka sasa mikoa yote ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar imethibitisha kushiriki isipokuwa mikoa minne ambayo leo sitaitaja kwa kuamini kuwa ndani ya siku chache itathibitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.
(Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante kwa wasilisho lako, Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA –KATIBU MEZANI: Miswada ya Sheria ya Serikali

MWENYEKITI: Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali
(Na. 4) wa Mwaka 2018 *(The Written Laws Miscellaneous
Amendments (No. 4) Bill, 2018)*

Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania wa Mwaka 2018 (*The Tanzania Meteorological Authority Bill, 2018*)

Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri wa Ardhini wa Mwaka 2018 (*The Land Transport Regulatory Authority Bill, 2018*)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018 (*The Political Parties (Amendments) Bill, 2018*)

Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 (*The Water Supply and Sanitation Bill, 2018*)

(*Kusomwa Mara ya Kwanza*)

MWENYEKITI: Ahsante, miswada hii imesomwa mara ya kwanza na kwa mujibu wa Kanuni itapangiwa na Mheshimiwa Spika ipelekwe kwenye Kamati husika.

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha wa Mwaka 2018 (*The Microfinance Bill, 2018*)

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

(*Majadiliano Yanaendelea*)

MWENYEKITI: Ahsante, jana tulikamilisha wachangiaji wote na kwa leo mtoa hoja anapata fursa sasa ya kuhitimisha hoja yake lakini kwa kufafanua yale ambayo mlishauri kwenye muswada huu lakini tutaanza na Mheshimiwa mmejipangaje; Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali,

lakini kabla AG hujaanza niwashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge kwa msaada mlionipa, katika hatua hii Mheshimiwa Spika anakuja kwenye kiti. (*Makofi*)

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

SPIKA: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali tafadhali, robo saa.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kuwa mchangiaji wa kwanza katika kuhitimisha hoja iliyopo mbele yetu. Mimi nitajikita zaidi kwenye masuala ya Kikatiba na kisheria.

Mheshimiwa Spika, nikianza na suala la Kikatiba kuliibuka hofu na wasiwasi kidogo miongoni mwa wachangiaji waliochangia jana kwamba sheria hii kama tukiipitisha itakuwa inavunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu inahusisha mambo ya *microfinance* na kwa maoni ya wachangiaji hao kwamba haya mambo nadhani ni sehemu ya masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mtazamo wake ni kwamba masuala haya ya *microfinance* siyo sehemu ya masuala ya Muungano na hilo nimeli-*confirm* kwa kuzungumza na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar. Baada ya kusema hivyo sasa naomba nijielekeze katika hoja zilizotolewa zikionesha wasiwasi huo kwamba masuala haya ya *microfinance* ni masuala ya Muungano na kwa jinsi hiyo Bunge hili linaweza kuwa pengine halikufuata njia sahihi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza iliyotolewa ni kwamba haya masuala ya *microfinance* yanahusu fedha na fedha ni suala la Muungano lakini hoja hii imetokana na kuangalia ile nyongeza ya kwanza katika nyongeza za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na orodha ya 12 katika nyongeza hiyo ambayo inabidi sasa labda tuangalie tafsiri zote ya kiswahili na ya kiingereza. Katika tafsiri ya kiswahili au

katika Katiba hii *version* ya kiswahili inazungumzia juu ya sarafu na fedha kwa ajili ya malipo yoyote ambayo ni pamoja na noti. Kwa kuwa inataja neno fedha inaweza ikaleta *confusion* kidogo. Ukienda kwenye version ya kiingereza inazungumza juu ya *coinage and currency for legal tender including notes*. Sasa kama unavyoona hii inazungumza juu ya sarafu na noti na *concept* ya fedha ni pana zaidi kuliko sarafu na noti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa tafsiri ambayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali anatoa ni kwamba neno fedha kama lilivyowekwa katika ile orodha ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kile kipengele cha 12 inahusiana na sarafu na noti na haihusiani na huduma za kifedha.

Mheshimiwa Spika, hapa pia ilitolewa wasiwasi mmoja kwamba tunayo Sera ya taifa kuhusu fedha ambayo ni sera ya Muungano lakini niseme tu na kwa heshima kabisa kwamba hii ni sera na sera haiku juu ya Katiba, kwa hiyo Katiba inaanza halafu inakuja sera. Kwa hiyo, sera inaweza kuwa imezungumza hivyo lakini kwa sababu Katiba imezungumza tofauti basi sera haiwezi ikawa juu ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia na hoja nyingine katika suala hilo hilo la Katiba kwamba mabenki ni suala la Muungano na kama ni suala la Muungano basi sheria hii pengine itakuwa inavunja Katiba. Hoja hiyo pia ilijikita katika ile ile nyongeza ya kwanza inayopatikana katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kile kipengele cha 12.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia tafsiri ya neno benki katika Sheria ya Benki Kuu na pia katika Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha, utagundua kwamba yapo mambo mengi yaliyomo katika huu wigo wa huduma ndogo za fedha (*microfinance*) ambayo yapo nje ya ile *concept* ya benki kadri ilivyowekwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, kwa kuwa hayo mambo yapo nje ya wigo huo, huwezi ukasema kwamba ni sehemu ya mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, lakini pengine baada ya kusema haya, niseme kwamba sheria hii kadri ilivyopangwa itatumika Tanzania Bara. Na tukienda katika Ibara ya 64(1) na hata 64(3) inazungumza waziwazi kwamba Bunge hili linayo mamlaka ya kutunga sheria katika masuala yoyote yasiyo ya Muungano ambayo yanahusu Tanzania Bara na kwa hiyo nadhani Bunge hili linafanya sahihi kutunga sheria katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, palikuwa na wasiwasi mwingine unaohusiana na mamlaka ya Benki Kuu, kwamba Benki Kuu ni jambo la Muungano na pengine Benki Kuu itahusika katika usimamizi wa sheria hii. Hiyo hoja kwamba Benki Kuu ni suala la Muungano inatokea pia katika nyongeza hiyohiyo ya kwanza, katika orodha ile ya mambo ya Muungano kipengele cha 12, na pia kuna ukweli kwamba tuna Sheria ya Benki Kuu ambayo ni sheria ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, tunavyofahamu Benki Kuu kimsingi ni taasisi ya usimamizi wa masuala yote ya fedha na kwa hiyo inategemewa kwamba itasimamia hizi shughuli za huduma za fedha kwa upande wa Tanzania Bara. Na Sheria hiyo ya Benki Kuu inatumika pia upande wa Zanzibar. Sasa kwa misingi hiyo Zanzibar haiwezi kutunga sheria ambayo itakwepa mamlaka ya Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, nirudie tena hapo; Zanzibar haiwezi kutunga sheria ambayo itakwepa mamlaka ya Benki Kuu, vinginevyo likitokea jambo hilo itakuwa ni kuvunja Katiba, Ibara ya 64(3). Na kwa hiyo, Benki Kuu itaendelea kuwa na mamlaka ya kusimamia mambo ya fedha hata kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na jambo la pili ambalo lilikuwa ni la kisheria, hili ni suala la *individual money lenders*, wale wakopeshaji binafsi, na ilikuwa inaonekana kwamba hawa pengine hawajaguswa na sheria hii. Ninapenda tu nikuthibitishie na kukuhakikishia kwamba katika ile *further schedule of amendments* iliyoletwa leo jambo hili limeingizwa

na kwa hiyo sasa hawa *individual money lenders* na wao sasa watakuwa wanasimamiwa vizuri na sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia na suala la wakopeshaji katika mazao, nalo hili kwa kadri ya michango iliyotoka jana lilionekana kwamba halijawekwa sawasawa katika sheria hii. Naomba katika hilo niseme kwamba kwa hii nyongeza ya mabadiliko iliyoletwa leo na Mheshimiwa Waziri wa Fedha hawa sasa nao wameguswa na sheria.

Mheshimiwa Spika, na jambo la nne ninaloliona pia ambalo lilikuwa kubwa, suala la umuhimu wa kudhibiti riba na namna ya kushughulika na vile vipengele vya mikataba visivyoya utu, tunaweza tukasema *unconscionable terms*, katika ile mikataba ya kukopeshana. Kwa kadri ya michango mbalimbali ya Wabunge kulikuwa na wasiwasi kwamba sheria hii pia haijalitazama eneo hili au kuwatazama hawa wakopeshaji wa aina hiyo kwa kiwango kinachotakiwa. Na katika hili nalo nikuhakikishie kwamba katika hii *further schedule of amendment* iliyoletwa na Mheshimiwa Waziri, jambo hili pia nalo limekuwa *covered*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maelezo yako mazuri kwenye suala hilo. Sasa nimuite mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mpango, karibu sana, una nusu saa hivi. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kwanza kukushukuru wewe binafsi, lakini pia Mheshimiwa Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha vizuri mjadala huu kuhusu Muswada wa Sheria ya Sekta Ndogo ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutambua michango iliyotolewa na Kamati ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene,

Mbunge wa Kibakwe na Waheshimiwa Wabunge wote waiochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi hapa Bungeni. Ninawashukuru wote kabisa kwa dhati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nichukue fursa hii ya kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Adelardus Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kufafanua vizuri baadhi ya hoja na hususani zile za kisheria na Kikatiba na pia zile za kiuandishi wa sheria. Aidha, ninamshukuru sana Bi. Sara Barahomoka, Mwandishi Mkuu wa Sheria, na wataalam wake kwa kazi nzuri sana waliyoifanya usiku na mchana kwa kushirikiana na wataalam wa Wizara yangu ya Fedha na Mipango, Benki Kuu ya Tanzania na Tume ya Ushirika wakati wa kupokea michango ya Waheshimiwa Wabunge, kutayarisha majedwali ya marekebisho na majibu ya hoja mbalimbali; ninawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jumla ya Wabunge 27 wamechangia hoja niliyowasilisha. Kati ya hao 25 wamechangia kwa kuzungumza na wawili kwa maandishi. Kama nilivyoeleza, ninafarijika kwa michango mizuri sana iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wote. Kwa kweli kama mnavyofahamu Bunge hili katika siku 14 za Kikao hiki nimekuwa ninasimama hapa karibu kila siku. Michango ya jana ilinitoa uchovu kabisa, kwa hiyo, ninawashukuru na sasa naomba kueleza kwa muhtasari majibu ya hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kulikuwa na hoja kwamba Serikali ihakikishe kwamba pindi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itakapokuwa inaandaa Sera na Sheria ya Huduma Ndogo ya Fedha, basi Serikali ya Muungano wa Tanzania ishiriki kikamilifu ili kuhakikisha kwamba hakutakuwa na ukinzani katika udhibiti na usimamizi wa huduma ndogo za fedha. Serikali inaupokea ushauri huu na tutauzingatia.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, Kamati ya Bajeti ilikuwa na pendekezo kuhusu tafsiri ya neno *community microfinance group* kama ambavyo walifafanua kwenye

kitabu cha maoni na ushauri wa Kamati. Naomba tu niseme kwa kifupi kwamba Serikali inakubaliana na mapendekezo ya Kamati na tumefanyia kazi tafsiri hiyo kupitia aya (b) ya jedwali la marekebisho. Hata hivyo, baadhi ya maeneo yamefanyiwa marekebisho kwa lengo la kuhakikisha kwamba tafsiri inayopendekezwa haiathiri utekelezaji wa sheria hii kwa watoa huduma wa daraja la nne. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu ambayo ilitolewa na Kamati ni mapendekezo ya neno *micro leasing*, kwamba irekebishwe kwa kutumia uwiano wa thamani ya mali kwa mtaji (*ratio of total assets to co-capital*) badala ya kutaja kiwango cha shilingi milioni 10. Tafsiri ya neno *micro leasing* imezingatia matakwa ya sheria ya Fedha na Karadha (*Financial Leasing Act, 2008*) na Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342.

Mheshimiwa Spika, pamoja na dhamira njema ya Kamati ya kutafsiri neno hilo kwa kutumia *ratio of total assets to co-capital*, kigezo cha *co-capital*/kinatumika kwa mabanki yanayofanya biashara ya benki (*banking business*) ambapo taasisi ndogo za fedha ambazo hazifanyi biashara ya benki hazina uwezo na mifumo ya kukokotoa *co-capital* muda wote (*at any time*). Hivyo, tafsiri iliyotolewa kwenye kifungu hiki ni ile ambayo ni rahisi kwa taasisi ndogo za fedha kuitumia.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nne ya Kamati ilikuwa ni ushauri kwamba Serikali iongeze kifungu kidogo cha (iv) ili kuweka mazingira ya kusajili na kuvitambua vikundi vilivyopo katika huduma ndogo za fedha ambavyo havina sehemu maalum ya kufanyia biashara. Serikali imepokea ushauri huu wa Kamati na kuufanyia kazi na katika jedwali la marekebisho tumeweka kifungu kipyaa cha 59(a).

Mheshimiwa Spika, hoja ya tano, Kamati ilishauri utolewaji wa leseni usiwe chanzo cha kukwamisha utolewaji wa huduma ya mikopo katika SACCOS. Niseme tu kwamba ushauri huu umepokelewa na tutaufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati iliishauri kwamba Waziri mwenye dhamana na huduma ndogo za fedha atunge Kanuni mapema iwezekanavyo ili ziwezeshe utekelezaji bora wa sheria hii mara itakapopitishwa na Bunge. Ushauri huu wa Kamati nao umepokelewa na tutauzingatia, na ninapenda niliahidi Bunge lako Tukufu kwamba mara baada ya Bunge lako kuupitisha Muswada huu nitawaagiza wataalam wa Wizara yangu waanze kazi ya kuandaa kanuni za sheria hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati pia iliishauri Serikali kuhakikisha kwamba pamoja na kuwalinda watumiaji wa huduma ndogo za fedha ni lazima pia kuweka mazingira ya kuwalinda watoa huduma dhidi ya wakopaji ambao kwa makusudi hawataki kurejesha mikopo waliyochukua. Miongoni mwa madhumuni ya sheria hii ni kuongeza imani ya matumizi ya huduma ndogo za fedha kwa kuwalinda watumiaji wa huduma hizo. Aidha, misingi ya kuwalinda walaji (*principles of consumer protection*) katika Sekta ndogo ya Fedha haihusishi kuwalinda watoa huduma ndogo ya fedha kwa kuwa kuna sheria mbalimbali za nchi zinazoweza kutumiwa na watoa huduma ndogo za fedha kulinda haki zao.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilibaini kuwa muswada huu haujatoa tafsiri ya maneno *commodity lenders*, na walitushauri tulifanyie kazi mapema ili kuwalinda wananchi wa kipato cha chini ambao wamekuwa wakinyonywa na mfumo huu. Kama Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali alivyokwisha kueleza, tumelifanyia kazi kupitia aya za (a), (b) na (e) kwenye jedwali la pili la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, na mwisho, Kamati iliishauri Serikali ihakikishie utekelezaji wa sheria unakwenda sambamba na uelimishaji wa umma juu ya malengo ya sera na sheria ambayo inatungwa. Huu ni ushauri muhimu sana na Serikali itahakikisha kwamba wananchi wanaelimishwa kuhusu malengo ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017 na sheria ambayo inapendekezwa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niende kwenye baadhi ya hoja ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia kwa kuzungumza. Nikianza na Mheshimiwa Hussein Bashe ambaye alisema sheria inayopendekezwa inatumika Tanzania Bara pekee na tuhakikishe kuwa Serikali inashirikishwa katika zoezi la kuandaa Sera na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha kwa upande wa Zanzibar ili pasiwemo mgongano wa kisheria. Hili tayari Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amekwishalitolea maelezo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mheshimiwa Bashe alisema maneno *community microfinance groups* yarekebishwe ili vikundi vya kijamii visivyofanya biashara visihusishwe na sheria hii. Tumefanya marekebisho kupitia aya ya (b) ya jedwali la marekebisho lililowasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mheshimiwa Bashe alieleza kwamba kanuni zitakazotungwa chini ya sheria hii zipitiwe na Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo kabla ya kusainiwa. Niseme tu kwamba *this is good practice*, Serikali inapokea ushauri na tutatekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Upendo Peneza alitoa hoja kwamba baadhi ya vifungu vimebainisha kwamba adhabu zitawekwa kwenye kanuni na utekelezaji wa vifungu hivi utakuwa ni mgumu na pia kuna sehemu nyingi zimeonesha kuwa mamlaka ya usimamizi itafanya itakavyoona inafaa. Napenda niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba vifungu hivi vimeshafanyiwa marekebisho kupitia aya ya (e) ya jedwali la marekebisho lililowasilishwa na Serikali. Aidha, adhabu ya jumla kupitia kifungu cha 51 kitatumika kwa vifungu ambavyo havijaainisha adhabu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Peneza pia alieleza kwamba watoa huduma katika daraja la nne waondolewe kwenye sheria hii badala yake Serikali iandae mwongozo wa kusimamia vikundi hivi kupitia halmashauri. Chimbuko la sheria hii ni utekelezaji wa Sera ya Huduma Ndogo ya Fedha ya Mwaka 2017, na sera hiyo inatambua watoa huduma katika

madaraja yote ikiwemo daraja la nne. Aidha, sheria inaweka utaratibu wa kusajili na kuratibu shughuli za watoa huduma wa daraja la nne kwa lengo la kuwatambua, kuwawezesha, kupata takwimu na kulinda watumiaji wa huduma husika.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kupitia jedwali la marekebisho, Serikali imeweka sehemu mahususi inayoainisha utaratibu wa kusimamia daraja la nne. Sheria hii imebainisha kwamba kutaandaliwa kanuni na miongozo mahususi kwa ajili ya kusimamia daraja la nne.

Mheshimiwa Spika, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Mashimba Ndaki, alitushauri kwamba Serikali ihakikishe Benki Kuu na mamlaka kasimiwa zinapewa rasilimali watu na bajeti ya kutosha ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yaliyo chini yao. Tunaupokea ushauri huu na tutauzingatia.

Mheshimiwa Spika, lakini pia alishauri Serikali ihakikishe kuwa mamlaka kasimiwa chini ya sheria hii zipewe elimu ya kutosha kuhusu majukumu yao ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa sheria hii. Niseme tu kwamba Serikali itahakikisha kwamba kabla ya kutekeleza sheria hii elimu ya kutosha inatolewa kwa mamlaka kasimiwa kwa lengo la kuziwezesha kutekeleza majukumu yao chini ya sheria hii ambayo inapendekezwa. Kwa hiyo, tunaupokea ushauri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mheshimiwa Ndaki alitushauri kwamba tufanye utafiti wa kutosha wa huduma ya *commodity microfinance* na tulete marekebisho ya sheria inayopendekezwa. Mwanasheria Mkuu wa Serikali hili pia amelieleza. Niseme tu kwamba kupitia aya za (a), (b) na (f) la jedwali la pili la marekebisho, inapendekeza marekebisho ya Muswada ili kuingiza dhana ya *commodity microfinance* na Serikali itafanya utafiti kama Mheshimiwa Ndaki na Kamati ya Bajeti walivyotushauri na ikibidi basi tutaleta marekebisho ya sheria Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Heche yeye alisema sheria hii inalenga watoa huduma ndogo za fedha kwa lengo la kuwatoza kodi hapo baadaye. Napenda nisisitize tu, kwamba madhumuni ya sheria hii ni kuwatambua watoa huduma ndogo za fedha kwa lengo la kuwasimamia, kupata takwimu, kuwalinda na kuwawezesha watumiaji wa huduma ndogo za fedha.

Mheshimiwa Spika, mchango mwingine ulitoka kwa Mheshimiwa Catherine Ruge na yeye alianza na tafsiri ya maneno biashara ya huduma ndogo ya fedha kwamba haijitoshelezi kwa dalaja la nne. Na hivyo ilishauriwa watoa huduma ndogo za fedha katika daraja hilo waondolewe katika sheria hii na Serikali iande mwongozo wa kusimamia daraja hilo. Nimekwisha lifafanua hili kwamba chimbuko la sheria hii ni kutekeleza sera yetu ya mwaka 2017 ambayo inayatambua madaraja yote.

Mheshimiwa Spika, pili, Mheshimiwa Ruge alishauri kwamba sheria haijaainisha jukumu la uwekezaji, uwezeshi, na utoaji elimu kama moja wapo ya majukumu ya Benki Kuu chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kupitia aya ya (u) ya jedwali la marekebisho utaratibu wa uwezeshaji na utoaji elimu kama moja wapo ya majukumu ya Benki Kuu kwa kushirikiana na Balaza la Taifa la Uwezeshaji wananchi kiuchumi chini ya sheria hii umeainishwa. Mheshimiwa Ruge pia alisema mamlaka kasimiwa hawana uwezo wa kifedha na rasilimali watu kuweza kutekeleza majukumu waliyo kasimiwa kusimamia daraja la nne.

Mheshimiwa Spika, naomba nilitaarifu Bunge kwamba Serikali imejipanga fedha kwa ajili ya utekelezaji na usimamizi wa daraja la nne, na mwongozo kwa ajili maandalizi ya bajeti ya 2019/20 imetoa maelekezo kwa halmashauri zote kutenga fedha kwa ajili ya kazi hii. Ushauri wa nne wa Mheshimiwa Ruge ilikuwa ni kwamba utaratibu wa kuandaa vitabu vya hesabu ufanywe kwa kuzingatia viwango vya kitaifa badala

ya viwango vya kimataifa, maoni haya tumeyazingatia kupitia aya ya (y) ya jedwari la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine ulitoka kwa Mheshimiwa Shally Raymond, na moja alisema je, Benki Kuu iko tayari kutoa mafunzo na kuwajengea uwezo watendaji wa mamlaka kasimiwa hasa halmashauri kuwawezesha kusimamia majukumu vizuri chini ya sheria hii. Mkakati wa huduma jumuishi za kifedha yaani *National Finance Inclusion framework* umeainisha majukumu ya Benki Kuu na ya wadau wengine ikiwa ni pamoja na yale ya kutoa mafunzo na kuwajengewa uwezo Watendaji wa Mamlaka mbalimbali zinazohusika na usimamizi wa Sekta Ndogo ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Raymond pia alisema aliuliza kama watu wa chini hasa waliopo kwenye vikundi kama watapata elimu kuwawezesha kuhusu huduma hii na fursa zilizopo. Kama nilivyokwisha sema aya ya (u) ya jedwari la marekebisho tumeweka utaratibu wa kuiwezesha benki kwa kutoa elimu kwa watumiaji wa huduma ndogo za fedha na hasa vikundi vya kijamii kwa lengo la kunufaika na fursa zilizopo. Lakini pia aliua kwa kuwa mabenki yatafaidika na daraja la nne kupitia amana ambazo wanaziweka kwenye mabenki je watasaidiwa katika kulea na kukuza watoa huduma wa daraja la nne.

Mheshimiwa Spika, sheria hii inaainisha shughuli mbalimbali zinazoweza kufanywa na mabenki na Taasisi za fedha ambazo zinaweza kusaidia kulea na kukuza watoa huduma wa daraja la nne na miongoni mwa shughuli hizo ni pamoja na utoaji wa mikopo kwa masharti nafuu na elimu ya fedha.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine zilitolewa na Mheshimiwa Janet Mbene ambaye kwanza aliuliza juu ya viwango vya mitaji vitakavyoainishwa kupitia kifungu cha 9 cha sheria kwamba viwe na ulingano. Kanuni zitakazotungwa chini ya sheria hii zitaainisha viwango vya mitaji kwa kuzingatia watoa huduma wa daraja husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Janet aliuliza kwamba tuainishe adhabu kwenye vifungu vya sheria ili ziweze kujadiliwa na Bunge na kupitishwa ili ziweze kutekelezeka. Niseme tu kwamba vifungu hivi tumeshavifanyia marekebisho kupia jedwari la marekebisho lillilowasilishwa na Serikali. Aidha, adhabu za jumla kupitia kifungu cha 51 itatumika kwa vifungu ambavyo havijaainishwa adhabu. Mheshimiwa Janet aliuliza pia kama Taasisi za huduma ndogo za fedha zitahama madaraja kwa utaratibu gani? Ibara ya 11 ya Muswada imeweka vigezo vya msingi vya kuzingatia ikiwemo mahitaji ya mtaji, idadi ya wanachama au wateja aina ya shughuli zinazofanywa nakadhalika, aidha utaratibu wa kuhama madaraja utaaainishwa kupitia kanuni chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbene pia aliuliza kama Taasisi za huduma ndogo za fedha zitaweza kulipa gharama za usimamizi wakati Benki Kuu itakapolazimika kufanya hivyo. Niseme tu kwamba Taasisi za huduma ndogo za fedha hazitatozwa fedha kugharamia majukumu ya Benki Kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Japhary Michael alikuwa na hoja kubwa mbili, moja kwamba sheria iwatabue wakopeshaji binafsi na kuwawekea utaratibu wa kuwawezesha kufanya shughuli zao. Na pili kwamba sheria itengeneze mfumo mzuri kwa watoa huduma katika daraja la nne kuwawezesha kulipa kodi. Kwa lile la kwanza Mheshimiwa *Attorney General* amelieleza lakini niseme tu tena kwamba aya ya (a), (c) na (e) ya jedwari la pili la marekebisho tumefanya marekebisho ili kuingiza dhana ya ukopeshaji binafsi na kanuni zitaweka utaratibu mzuri wa namna wakopeshaji binafsi watakvoyofanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, na lile la pili madhumuni ya sheria hii kama nilivyokwisha sema lengo letu ni kuwatambua watoa huduma ndogo za fedha ili tuweze kuwasimamia tupate takwimu, tuwalinde na kuwawezesha watumiaji wa huduma hizi ndogo za fedha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa King maswali yake kimsingi yamejibiwa katika ufafanuzi wa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Lakini kimsingi tumeyapokea, labda tu niseme moja alisema sheria ya udhibiti wa fedha haramu ni ya muungano na chombo chenye dhamana ya kudhibiti fedha haramu ni cha muungano na swali lake ilikuwa ni je, Serikali itatumia utaratibu gani kudhibiti fedha haramu katika sekta ya huduma ndogo za fedha kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba sheria ya udhibiti wa fedha haramu sura 423 si ya Muungano Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ina sheria yake ya udhibiti wa fedha haramu ambayo inaitambua *financial intelligency unit*. Aidha miongoni mwa matakwa ya sheria ya huduma ndogo ya fedha ni pamoja na kuelekeza Taasisi na watumiaji wa huduma ndogo za fedha kuzingatia sheria udhibiti wa fedha haramu. Aidha ni matarajio yetu kwamba sheria ya huduma ndogo za fedha itakayotungwa Zanzibar italenga kuhakikisha kwamba matakwa ya sheria ya udhibiti wa fedha haramu ya Zanzibar yanazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Madgalena Sakaya aliuliza juu ya fedha za desi kama zinaweza kupatikana na kurejeshwa kwa wananchi na kwa utaraibu gani? Sheria inalenga kusimamia na kudhibiti biashara ya huduma ndogo ya fedha pamoja na kuwawezesha watumiaji na watoa za fedha, suala la fedha za desi si miungoni mwa maudhui ya sheria hii kwa kuwa lilijitokeza kabla ya kutungwa kwa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Msigwa yeye aliuliza utaratibu gani utatumika kuwadhibiti wakopeshaji binafsi na kuwaweza kuingia kwenye mfumo rasmi. Hili nimekwisha litolea maelezo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Njeza alitushauri kwanza aliuliza je mabanki yayoanzishwa kwa ajili ya kutoa huduma ndogo za fedha wako kwenye daraja gani? Mabanki yenye lengo la kutoa huduma ndogo za fedha ni miongoni mwa Taasisi zinazoweza kutoa huduma hizo chini

ya daraja la kwanza. Lakini pia aliuliza katika utungaji wa kanuni Wizara iangalie riba zinazotozwa kwa watoa hudumua ndogo za fedha, hili tumekwisha kulitolea maelezo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mtulia yeye aliuliza kuhusu makampuni ya simu kama yataingizwa kwenye sheria hii. Sheria hii inalenga kusimamia na kudhibiti biashara ya huduma ndogo za fedha pamoja na kuwawezesha watumiaji wa huduma hizo. Hivyo makampuni ya simu yenye lengo la kutoa huduma ndogo za fedha yatasimamiwa pia kupitia sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, alikuwa na hoja mbili kubwa moja, kama vikundi vya upatu ni miongoni mwa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha vitakavyosimamiwa chini ya sheria hii, na kama wakopaji wapewe elimu kuhusu ukopaji na sheria ya mikataba. Sheria hii ina lenga kusimamia na kudhibiti biashara ya huduma ndogo za fedha pamoja na kuwawezesha watumiaji wa huduma ndogo za fedha. Hivyo vikundi vya upatu haviwezi kusimamiwa chini ya sheria hii kwa sababu havijihusishi na biashara ya huduma ndogo za fedha.

Mheshimiwa Spika, na kwa lile la pili tunapokea ushauri, sheria hii pamoja na mambo mengine imeainisha taratibu za kuwalinda watuaji wa huduma ndogo za fedha ikiwa ni pamoja na kuwapa elimu ya fedha na masuala ya udhibiti wa mikataba ya wakopaji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kamala naye alisema tuangalie suala la riba kwa umakini na hili nimekwisha kulitolea maelezo. Lakini pia aliuliza Benki Kuu imejipangaje kutumia sheria hii kujenga *a credit economy*? Kujenga *credit economy* kuna husisha kuweka mazingira mazuri kwa wananchi, kutumia mikopo kutoka vyanzo mbalimbali katika shughuli za kujenga uchumi badala ya kutumia fedha kutoka kutoka vyanzo binafsi.

Mheshimiwa Spika, eneo hili limekuwa ni changamoto na ni moja ya sababu ya kutokopesheka kwa sababu ya

viatarishi mbalimbali vikiwemo vya kutotambulika na kukosa dhamana, na viatarishi hivi vimepelekea mifumo ya fedha kuweka masharti magumu ya kufikia mikopo katika mfumo wa mabengi. Na kwa kutambua changamoto hizi na umuhimu wa kujenga *credit economy* Serikali imefanya jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja kurasimisha rasilimali za wananchi ili zitumike kama dhamana, kuandaa vitambulisho vya taifa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu kwa upande wake imeendelea kuchukua hatua za kuongeza ukwasi kwenye uchumi. Na kwa hatua hizi pamoja na mwendelezo wa elimu kwa Umma Serikali inaendelea na zoezi la vitambulisho vya Taifa na matarajio yetu ni kwamba riba zitaanza kuakisi uhalisi wa gharama za mikopo nchini. Mheshimiwa Ndasa yeye alitushauri kwamba kanuni zitakapotegenezwa ziwe rafiki kwa makundi yote, tunaupokea ushauri huu na tutauzingatia wakati wa kuandaa kanuni.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbaraka Dau alisema Benki Kuu itakapo kasimu mamlaka yake kwa mamlaka kasimiwa ihakishe inatanga kupitia gazeti la Serikali. Tumezingatia hili kupitia kifungu cha 14(1). Haki ya rufaa isiishie kwa Waziri peke yake tunakubaliana na tumezingatia kupitia aya ya (m) na (p) ya jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Kiruswa alileta mchango kwa maandishi na yeye daraja la nne linaruhusu vikundi vya kijamii vinavyotoa huduma ndogo za fedha litungiwe kanuni nyepesi. Lakini pili watoa huduma ndogo za fedha kwa daraja nne wasilazimike kuomba leseni tumepokea ushauri na tutauzingatia wa kuandaa kanuni lakini pia sheria haina takwa la kisheria kwa watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la nne kuomba leseni.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Felister Bura yeye alisema je, wafanyakazi watasaidiwaje baada ya Taasisi au kikundi kufa. Wafanyakazi watasimamiwa na sheria za kazi na ajira na sheria nyingine zilizopo, Mheshimiwa Dkt. Kafumu

yeye alikuwa na hoja kuhusu vikundi vilivyopewa fedha kwa lengo la kusaidia na vikundi vya kidini...

SPIKA: Malizia tu Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa marekebisho yaliyanyika kupitia aya ya (b) ya jedwari la marekebisho, vikundi vya aina hii havitahusishwa kwenye sheria hii, nina washukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu ya kuboresha Muswada huu, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango tunashukuru sana kwa kutoa hoja na hoja imeungwa mkono. Tunakushukuru sana kwa maelezo uliyoyatoa, najua muda haukuwa unatosha lakini umejitahidi kutujibu wengi kabisa iwezekanavyo wale ambao tuliweza kuchangia, tunakushukuru sana, Katibu. (*Makofi*)

NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

SPIKA: Kamati ya Bunge Zima.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae, natumaini Waheshimiwa tunazo *amendments* mbalimbali ili iwe rahisi sana kwetu kuweza kwenda kwa haraka, sasa, Katibu tuanzishie.

NDG. JOSHUA CHAMWELA-KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kamati yako ielekeze kwenye Muswada wa sheria ya Huduma Ndogo za Fedha wa mwaka 2018 ukurasa wa tano.

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisha yake)*

Ibara ya 2

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anatropia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nilileta mapendekezo yangu nikitaka Muswada usome kwamba *this act should apply to Mainland Tanzania and Zanzibar* na mapendekezo hayo nimeyaleta kimsingi na nimesikiliza maelezo ya AG. Sielewi ni kwa kiwango gani anasema mambo ya *microfinance* siyo mambo ya Muungano na ameenda mbali zaidi akasoma nyongeza ya 22 akaidadavua vyema, ni masual gani yanayojikita katika Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naweza kumshauri nane kwamba masuala yanayohusiana na *microfinance* siyo masuala ya Muungano, na ukizingatia hiyo nyongeza ambayo ni kipengele cha 12 kinajitanabaisha dhahili kwamba mambo yote yanayohusiana na sarafum mambo ya benki, mambo mengine kadha wa kadhaa, na haya mambo kwenye *Tier 1* mpaka 3 unaona kwamba ni watu wanawekeza fedha zao wengine hata wana-*save*, mfano, *Tier 1* wana-*save*. Kwahiyo kama wana-*save* ni kama benki, *it is a mini Bank* kwahiyo sasa mnatumbiaje kwamba haya mambo siyo ya muungano? Kwa hiyo, ningepomba kipengele hicho hi Sheria iseme kwamba ita-*apply* Tanzania Bara na Zanzibar.

MWENYEKITI: Mwashasheria Mkuu walifafanua hili jambo labda ufafanuzi zaidi.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ufafanuzi zaidi ya nilioutoa. Nilisema neno "fedha" kama lilivyotumika katika nyongeza ya kwanza ile orodha ya 12 inahusu sarafu na noti peke yake, haigusi

huduma za fedha. Nikasema pia neno "Benki" kama lilivyowekwa katika hiyo hiyo nyongeza ya kwanza, orodha ya 12 lakini imetafsiriwa sasa katika Sheria ya Benki kuu na Sheria na Mabenki na Taasisi za fedha kuna mambo yaliyo katika *microfinance* ambayo haya -fit kwenye hiyo definition. Kwa hiyo, kwa msingi huo mambo ya *finance* kwa kweli kwa ujumla siyo sehemu ya masuala ya Muungano.

MWENYEKITI: Anatropia Theonest.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kama si karibia nitaomba wasomi wenzangu wanisaidie ambao walioko hapa au wenye uelewa wa kiwango hicho waniambie. Je, umesema mwenyewe Zanzibar kama Zanzibar kwa vile umesema mambo ya *microfinance* siyo masuala ya Muungano, Je, Zanzibar wanaweza kuanzisha kitu kama hichi na kika-*apply* Zanzibar? Akisema ni sawa kwamba na Zanzibar wanaweza kuanzisha kitengo chao cha fedha na kikakubalika ndani ya Zanzibar na kisihitaji kusimamiwa na Benki kuu au kisimamiwe na Benki Kuu *then* sina shida lakini kama anajua wkamba tunahitaji usimamizi wa Benki katika suala hili *then* lazima Benki kuu itamalaki Zanzibar na Tanzania Bara.

MWENYEKITI: Yaani sidhani kama nakuelewa kabisa.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, amenielewa kwamba...

MWENYEKITI: Kwa sababu hata kama alivyojibu AG kwamba hayo uliyoyauliza siyo ya Muungano lakini kama Benki ku ndiyo msimamizi kwa namna moja au nyingine, liwe la Bara litasimamiwa na Benki kuu, liwe la Zanzibar litasimamiwa na Benki kuu ni moja ndiyo maana nikasema sikuelewi unauliza nini. Hata kama Zanzibar wakianzisha kivyao bado Benki Kuu ni ile ile.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Benki kuu itasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Zanzibar wanaruhusiwa kuanzisha *microfinance* na ikasimamiwa na Benki kuu kama ambavyo Bara tumeamua kusimamia *microfinance* na ikasimamiwa na Benki kuu *then* sina shida. Lakini kama tunahitaji Benki kuu iwe moja isimamie huku na huku katika masuala yanayohusu fedha nadhani kun aumuhimu wa kuweka neno "Zanzibar" ili i-*apply* kote. Naamini nimeeleweka. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Yaani tumekusikia lakini hatujajua hoja yako ni nini. (*Kicheko*)

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Ameelewa, ambaye ninayemwambia ameelewa kwasbabau hija ninaitoa kwenye *speech* yake mweyewe akiwa anakataa kuonyesha kwamba huu Muswada unapaswa ku-*apply* Zanzibar.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Theonest unayemu-*address* ni Mwenyekiti wala siyo huyo unayesema ameelewa sijui ni nani.

Ibara ya 2

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 3

MWENYEKITI: Mheshimiwa Profesa ulitaka kusimama?
Ahsante

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nasimama kwa niaba ya Kamati ya Bajeti. Kwanza kabisa kumshukuru Mheshimiwa Waziri na AG kwa kuona kwamba kama marekebisho ya Kamati ambayo nadhani kila mtu anayo, ningeomba sana Waheshimiwa Wabunge kama mnayo yawe karibu na ukiangaia na *schedule* ya Serikali ambayo kusema kweli hatuna budi kushukuru kama Kamati ya Bajeti kwamba mapendekezo yetu mengi yamechukuliwa *on board* na kusema kweli

kumshukuru pia Mheshimiwa Waziri alipokuwa anahitimisha hapo ameonyesha kwamba pendekezo letu moja ambalo ni *item three* tayari amelikubali kuhusu upatu ila katika *amendments* zake haipo hiyo *section* inayohusu upatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama ikikupendeza niseme sasa yale mambo ambayo kama Kamati...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Profesa Upatu Kiingereza inaitwa nini?

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Ndiyo ni kama *revolving fund schemes*.

MWENYEKITI: Endelea Mheshimiwa.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *revolving fund scheme* kama kuna waingereza wazuri zaidi wanaweza wakasaidia pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Kamati ya Bajeti ambayo kwa kweli imeshirikiana sana na upande wa Mheshimiwa Waziri na timu yake kufika hapa tulipofika na kama tulivyokuwa tunachangia wengine wengi jana ni kwamba mantiki yetu na Sheria hii nzuri sana ilinde uhuru wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yetu yanalenga kuhakikisha kwamba uhuru wa jamii kuunda Taasisi ndogondogo za kuwasaidia kama ulivyo utamaduni wetu na inavyoendelea usije kwa namna fulani na bila kusudio kuathirika kwa sababu ya Sheria hii. Mheshimiwa Waziri ameleta *amendments* vizuri ila sasa ni *interpretation* na hapo labda AG atatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati tulipendekeza *item* ya kwanza ambayo inasema "*microfinance group does not include*" yaani *community microfinance group* inamaanisha hivyo kama inavyofafanuliwa kwenye Sheria lakini isihusishe wafuatao; *a community self-help group formed to receive collections from members all the nations for own social economic welfare and other safety net purposes as agreed among themselves.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *item* hiyo nashukuru kwamba Serikali imekuja na *concept* yetu lakini sasa kuna *negation* yake na hapa Mwanasheria labda atatusaidia kwa sababu anasema "*community sel-help group formed for safety net purposes and social economic welfare of members and which do not receive savings*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapo ndiyo tumekwama. Hivi vikundi hivi vya jamii kitu wanachokifanya ni kukusanya michango sasa *concept* ya *safety net* na *social welfare* utaitekelezaje kama hukusanyi michango (*savings*) yaani maana yake ni nini? *Whats is safety netting? Safety netting* ni watu kukusanya nguvu zenu pamoja kwamba jamani mtoto anakwenda shule karo haijatosha kuna kikundi cha wakinamama au wakinababa wasaidiana karo. Wanachokifanya hawa watu na ndiyo maana katika Kamati imetumia neno "*receive collections*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona ni muhimu sana kwamba neno "*receive*" *collections* liwe kusudi wanaotafsiri Sheria wasije wakaleta mambo yao mengine ambayo hayajakusudiwa, hilo ni la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali imekuja vizuri lakini tunaona kama kuna *negation* yaani ameweka lakini pia ametoa na mkono mmoja anachukua na mwingine anasema wasi-*receive*. *Do not receive savings and provide loans to its members*. Sasa mtoto wangu sina karo au mtoto yupo hospitali nakwenda kwa Mwenyekiti wa kikundi chetu nasema jamani ninahitaji laki moja lakini haki yangu labda kwa kikundi ni 50,000 nikopeshe na hii 50,000 nitakuja niweke

nguvu pamoja niweze kulipa baadaye. Kwa hiyo, vikundi hivi ndivyo vinavyoishi kwa hiyo sasa kama Sheria haisemi tuko katiuka hatari, hiyo ni *item* ya kwanza bila shaka itafafanuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na *item* ya pili ambayo ningependa kuonyesha; katika mawasilisho ya Serikali ana-*define special interest groups* kama Kamati ilivyosema. Kamati ilisema hizo *special interest groups, clubs and associations collecting financial contributions from members or receiving charity donations for enhancement of their own social economic welfare*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote hapa ni wawakilishi wa wananchi wakati mwingine kikundi kinakuomba mchango uwawezeshe kidogo. Wameshachanga za kwao na sisi tunafanya *donations* kwa hiyo, ni muhimu kwamba wawe na uhuru huo wa kupokea misaada midogo midogo wanayopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali ilikuja vizuri ila ilipokuja wenyewe wanasema "*special interest groups, clubs and associations collecting financial contributions, tuko pamoja, from members or receiving charity donations, tuko pamoja, formed sasa tunakuja kuachana wapi? Sasa wanaleta sharti jipya "and registered under the societies act for enhancement of their economic social welfare"*. Kwa hiyo, wanasema sas ahivi vikundi hivi vya kuchanga karo, vya kuchanga hela za hospitali kwanza viende kuanidishwa chini ya Sheria ya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo Sheria ya Ushirika hapa mkononi. Kuandikisha Ushirika kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika ni shughuli. Hivi vikundi hivi vya haraka haraka sasa itabidi waende chini ya *section 20*, kwanza *section 20* inasema "*Ushirika hauwezi kuwa na chini ya watu 10 au 20*" kwahiyu kuna masharti hayo yako hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu sasa ukienda *under part four* ya Sheria hi ambayo kwa muda huu niseme kwamba

wote tunaweza tukaipata kuna mlolongo mkubwa wa kuandikisha Ushirika lakini huko tunakotoka na Kamati iliona wananchi wanaandikishwa na Afisa Maendeleo ya jamii ndiyo wanaosajili hawa. Ni kitu anakuja, anawashauri, anawaandikisha na wanatambuliwa na ndiyo unaweza kwenda Benki kufungua *account* kwa mfano. Sasa ukisema waende chini ya Sheria ya Ushirika kwa kweli tutakuwa tumefungwa mikono. Wanawake watapata tabu, watu watahangaika, kwa hiyo nadhani siyo nia ya Sheria hii kwa hiyo ni *calibration* tu kusudi twende vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wka hiyo sisi tukafikiria kwamba hili pendekezo la Kamati na Kamati hii tulilikalia hili suala kwa kweli lilituchukulia muda sana lazima nikiri lilituchukulia muda sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Profesa muda sasa...

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Sawa, *sorry*.

MWENYEKITI: Nimekuvumilia kuvumilia kidogo sasa fanya *summary*.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho sasa karibu namalizia ahsante kwa kunivumilia lakini umuhimu wa suala hili utulinde linde katia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninakuja kwenye *point* ya mwisho kwahiyo hiyo nayo wataelezea lakini sisi tunaona kwamba pendekezo la Kamati halitofautiani sana na la Serikali ila la Serikali sasa linaleta sharti jingine ambalo litakuwa gumu sana kwa wale watu ambao tunawalenga kuwalinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upatu, Mheshimiwa Waziri ameshajibu, nililiuliza jana na amejibu vizuri amesema kwamba wanataka kulindwa sasa huwezi kumlinda upatu kama huchukui *item three* ya Kamati kwa Sheria ilivyokaa sasa hivi na sisi tumeikalia hapa kwa niaba yenu, tumeisoma

sana kwa hiyo tulikuwa tunaomba basi wa-*in corporate item three* iongezwe katika mapendekezo ya Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninafikiria kwamba kama hayo Serikali itatupa majibu au wakafikiria sisi kwa Kamati tunashukuru sana...

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Hapa tulipofika. Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Profesa. Hapa kuna hoja tatu na ziko wazi tu lakini tusikilize ufafanuzi ndiyo maana jana tulisema kwamba ni vizuri Kamati na Serikali mkaelewana lakini inaelekea hamjaelewana basi tutawasaidieni kuelewana. Mheshimiwa Waziri au Mwanasheria Mkuu? Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tunaposoma hii clause kadri ya amendments za Serikali ile *first schedule of amendments* ni vyema kuyasoma maneno yote yanayotangulia kabla ya vipengele (a), (b) na hicho kilichopendekezwa na Kamati hatujavijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukianza na maneno yaliyoko hapo, *clause 3*, tunakwenda (b) halafu hiyo *definition* na *community microfinance group, means "a group collectively formed and managed by members and registered under this Act to undertake microfinance business including mobilization of savings from its members and provisions of loans to its members"* hiyo ndiyo essence ya hiyo *community microfinance group*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yanafuata maneno "*but does not include*" sasa *concern* ya kwanza ya Mheshimiwa Prof. Tibaijuka, yale maneno "*which do not receive savings*

and provide loans” hiyo siyo kati ya vikundi ambavyo vitahusika katika hiyo *concept* ya *community microfinance group*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha pili cha (b) ana changamoto, *sorry*, ni hicho cha kwanza labda pia niongezee maneno hapo; ukikisoma hicho kifungu ukaenda mpaka mwisho wake inasema *“which do not receive savings and provide loans to its members for the purpose of undertaking microfinance business”* nilipenda ku-underline yale maneno *“for the purpose of undertaking microfinance business”* ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo *criteria* ya muhimu, kama inapokea hizo *savings* na inatoa *loans for the purpose of undertaking microfinance business* hiyo ni sehemu ya *community microfinance group*. Lakini kama inapokea *savings* na inatoa *loans, not for the purpose of undertaking microfinance business* hiyo siyo sehemu ya *community microfinance group*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani niliona niongeze kidogo maelezo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye *group (b)* ambayo ni *special interest groups* ambazo zimekua *formed and registered* nadhani kidogo pia alichanganya kwa sababu alifikiri tunazungumzia au tunaweka *requirement* ya *registration* lakini hizi ni *groups* ambazo...

MWENYEKITI: Mwanasheria Mkuu kidogo tu, tukuvumilie kidogo. Wale wa Kamati ya Bajeti tusaidiane msimuachie Profesa pake yake maana yake hili ni la Kamati siyo la Profesa pake yake. Hapa alivyoeleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali tunaanza kupata ile *“but not include (a), (b), (c)”* kwa hiyo maana yake (a), (b), (c) wala hazimo kama uelewa wangu ni sawa sawa. Sasa kama hazimo Profesa shida yenu ni nini kama Kamati kumbe hawa hawamo, sijui kama tuko pamoja!

MHE. PRF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sorry, Mwenyekiti wangu.

MWENYEKITI: Oohh Mheshimiwa Mwenyekiti.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na *response* yao ya marekebisho haya ya Kamati na maelezo mzuri sana yaliyoelezwa na Mheshimiwa Tibaijuka lakini ile *“does not include”* na *“which do not”* unapata *not not* mbili maana yake ni *positive* yaani kwenye *interpretation*. Kwa hiyo, yaani sasa nisikilize naiunganisha sasa, anasema *“ambayo haitahusisha haya masharti ya (a), (b), (c), (d) ambayo haitahusisha sasa tusome ndani; haitahusisha isipokuwa ndani yake kule tena inakamata.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema *“community self-help groups ambayo haihusishi community help-self groups formed formed for safety net purposes and social economic welfare of members and...yaani mpaka hapo hatuna shida ila “which do not receive savings” sasa huwezi ukawa na safety net ambayo haipokei kutoka kwa wanachama wake na huwezi kuwa safety net ambayo haitatoa mkopo au msaada huo tunaouzungumzia ndiyo shida hapo inapokuja. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo labda waingalie vizuri madhumuni hasa, ukishaiweka hivi tena maana yake ni kwamba vile vijikundi vidogo vidogo na pengine picha ya Serikali inaweza ikafikiri ile *saving* kubwa, hivi tunazungumzia vikundi vidogo vidogo sana vya jamii kwa nia ya kusaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shida ni usimamiaji wa Sheria. Hapa dhamira inaweza ikawa nzuri lakini kule Kongwa wakasema hii mnavunja Sheria lazima iitwe *microfinance business* sasa maana unairudisha kuwa *microfinance business* kwa hiyo wale watakuwa wanavunja Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hicho tu. (Makofi)

MWENYEKITI: Bado narudi kwako Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, uandishi wa sheria una tofauti kidogo siyo kama hesabu kwamba utatumia *formula* ya MAGAZIJUTO. Nakumbuka wakati ule tulikuwa tunaambiwa ukiweka *negative negative* au *positive positive* itakuwa nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kama nilivyosema yasomwe maneno mpaka mwisho, ukiyasoma mpaka mwisho ndiyo unapata maana. Inasema, *which do not receive savings and provide loans to its members for the purpose of undertaking microfinance business*, kinyume chake ni kwamba ambazo zina-*receive savings and provide loans but not for the purpose of undertaking microfinance business*. Hizi ndiyo zimekuwa *excluded*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Hiyo ni kwa lile la kwanza, la pili? Mheshimiwa mama Tibaijuka alikuwa na mambo matatu, lile la (b) na lenyewe linaishia hapo hapo? Hili la *registered under Societies Act for enhancement of their economic social welfare*.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hilo pia nitatoa maelezo yale yale. Mheshimiwa Tibaijuka asiwe *confused* na haya maneno *formed and registered and what not*, cha muhimu ni ile sentensi pale chini.

MWENYEKITI: *Microfinance business*.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: *Which does not include, kwa hiyo, this one is not included.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile la tatu.

MWENYEKITI: La tatu ni jipya kabisa nataka ulikubali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Hilo la UPATU.

MWENYEKITI: La *self-help groups*.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema, *self-help groups undertaking revolving schemes*, kwa heshima sisi tunafikiri kwamba hilo liko *covered* kwenye ile *item (i)* au *item (ii)*. Kwa hiyo, hakutakuwa na haja tena ya kuweka *a separate category* kwa sababu hii yote iliyozungumzwa hapa *self-help groups undertaking revolving schemes* inaingia vizuri sana kwenye *(i)* na au *(ii)*.

MWENYEKITI: Mtoa hoja Mheshimiwa mama Tibaijuka, naona umeridhika.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kwamba vikundi vinaruhusiwa kuchangishana, kukusanya hela ila hela hizo hazitakwenda kufanya biashara ya *microfinance*. Kama hivyo ndivyo ilivyo, maana yake ajue kwamba sheria nzuri pia lazima na sisi watu wa kawaida tuweze kuelewa, sasa angalia hii sheria mimi mwenyewe hapa niko *confused* na mwananchi wa kawaida itamuacha katika hali gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani katika *schools* za kuandika sharia, ni lazima pia lugha iwe nyepesi. Nataka kusema kama Mwanasheria ameridhika katika *final drafting* ieleweke jamani kwamba wanaruhusiwa sasa kukusanya fedha zao lakini sisi watu wa kawaida tulikuwa tunafikiria kwamba wamezuiliwa. Kama sisi humu ndani Waheshimiwa Wabunge hatujalipata sawasawa mtu wa kawaida huko kwenye Halmashauri si atanza kukimbizana na watu na marungu na kuwashika, ndiyo mantiki yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo ya Mwanasheria ambayo ni sehemu pia ya *Hansard* hapa, kama tukipata matatizo kwenye Halmashauri tutarejea kwamba *interpretation* ndiyo hii. Kama Mwenyekiti wangu akiniruhusu,

nadhani sisi Kama Kamati sasa tumeridhika tunaomba kuendelea. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mwanasheria Mkuu nimekuona umesimama.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, nimeona ni vyema nisimame na kulieleza hilo alilolieleza Mheshimiwa Tibaijuka. Katika mambo ambayo tumekusudia katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kuitafsiri sheria hii katika lugha ya Kiswahili mara moja itakapokuwa imepitishwa na kusainiwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mwanasheria. Kama alivyosema Profesa pale ni kwamba hii inakutaka usome mpaka nukta ya mwisho ndiyo upate picha. Watu wengi huwa tunakuwa wavuvi, tunaangalia ule mtiririko unajua hili haliruhusiwi lakini hii inataka uende mpaka uone ile *microfinance business* ndiyo upate picha nzima ya pale juu lakini ni stahili ya uandishi.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 4
Ibara ya 5

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 6

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anatropia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho yangu ni katika kifungu cha 6(2). Nataka kuondoa neno 'close' kwa maana ya akifunga biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza hilo eneo liondoke kwa sababu kuna sababu nyingi sana za mtu kufunga biashara na kifungu hicho kinamtaka atakavyofunga tu biashara aende kutoa taarifa. Kifungu kina *assume* kwamba mtu anaweza akafunga biashara *voluntarily*, kuna *circumstance* nyingi za kumfanya mtu afunge hii biashara. Ndiyo maana nimependekeza hilo neno '*close*' liondoke na kizalishwe kifungu kingine kidogo cha (3), ambacho kitamtaka kama anafunga biashara kwa sababu nyingine labda ameibiwa, janga la moto, yeye mwenyewe atoe taarifa, aandike barua apeleke kwa mamlaka inayosimamia akieleza kwamba nimefunga hii biashara na kwa kutoa sababu ya nini kimemkuta. Ndiyo marekebisho yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna marekebisho mengine madogo ya kifungu cha 6(3) ambayo sasa yanatoa *penalty* kule mtu ambaye amefeli kutoa taarifa. Nimeona kifungu kidogo cha (3) kinasema *penalty as prescribed in the regulations*. Hapa naona kama tumekwepa majukumu yetu badala ya kumuachia Waziri aende kutoa hizo adhabu kwenye kanuni sisi kama Bunge sasa tuamue tunatoa adhabu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimependekeza kwamba akishindwa kutoa taarifa ya kufunga biashara hiyo alipe faini ya *not less than five hundred thousand shillings and not exceeding one million shillings as the case of Tier 1 up to 3* kwa sababu ni biashara kubwa kidogo. Kwa *Tier 4* ambaye ni biashara ndogo kabisa, *a fine of not exceeding fifty thousand shillings* kama atakuwa amefunga biashara kwa sababu ambazo zimemkuta bila kutoa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo marekebisho yangu.

MWENYEKITI: Hili la mwisho sijui msingi wako ni nini lakini tuanze na lile la kifungu cha 6(2), Mwanasheria Mkuu, kwa nini mtu asiruhusiwe kufunga biashara kadri anavyoona inafaa, tufafanulie Mheshimiwa.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Muswada huu ni kudhibiti shughuli za huduma ndogo za fedha na mojawapo ya *aspect* ya huduma hizo ni kufungua pamoja na kufunga. Tumesikia hata kwenye michango ya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwamba mojawapo ya matatizo ni kutomjua huyo mtu yuko wapi au kile kitendo cha yeye kufunga ile biashara bila wateja wake kufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu sana katika sheria kumdhibiti wakati wa kufungua, wakati wa *operations* na ni lazima kujua kabla hajafunga maana tukimwachia hivi anaweza kufunga akatokomea kusikojulikana na tusijue tutampata wapi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mtu ana hela za watu halafu anaamua kufunga, anapotea tu na ana hela za watu, si lazima mtafuata kwenye *authorities* muulize huyu mtu mbona hatumuoni? Watakwambia si sheria Wabunge mlitunga kwamba mtu anajifungia tu, hatoi taarifa popote, tutajibu nini. Mheshimiwa Anatropia bado unatetea moja yako?

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachokifanya namsaidia mtunga sheria ili hili neno 'close' ambalo amelichomeka kwenye kifungu kidogo cha (2) sasa liwe *bold* katika kuzalisha kifungu kidogo cha (3). Sipingi kufunga ila neno hapa limechomekwa, nachotaka lipate maana na lipewe uzito. Ndiyo maana nikasema, nanukuu:-

" In the event a microfinance service provider closes a place of business for whatever reason, he shall have to submit a written notification to the Bank or Delegated Authority for so doing".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachokitaka ni kile kipengele ambacho kimechomekwa pengine kisieleweke hapa nakipa *meaning* kwa kuwa na kipengele chake maalum kwamba mtu atakapofunga biashara *for whatever reasons* amepata moto, ameibiwa, hicho kipengele

kinamsaidia aende kutoa taarifa kwa mamlaka husika. Mimi sikiondoe ila nazidi kuki-*bold* tofauti na yeye alivyofanya.

MWENYEKITI: Sasa Mheshimiwa Anatropia wao wanasema iwe unafungua, unafunga lazima utoe taarifa na maelezo yako ni *almost* kitu kile kile. Nadhani hilo halina shida tu-*deal* na hili linalofuata *unless* kama Waheshimiwa mnamuelewa mimi sioni kama kuna shida. Kifungu kinasema iwe unafungua, unafunga lazima utoe taarifa kwenye *relevant authorities* na wewe unasisitiza kama mtu akifunga atoe taarifa, kwa hiyo mnazungumza lugha moja tu, yaani wote mko pamoja mnachobishana ni Kiswahili tu. (*Makofi*)

MHE. ANATROPIA L. TEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jinsi neno lilivyochomekwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, twende kifungu kidogo cha (3) ambacho kinasema kwamba kutakuwa na *penalty as prescribed in the regulations*. Nachokitaka mimi *penalty* iwe *stated* hapa na siyo kuacha mamlaka kwa Waziri husika. Nikapendekeza *in case ya Tier 1* mpaka *Tier 3* ambayo ni *microfinance* kubwa faini yake iwe *clear* na sisi watunga sheria tuijue ni faini kiasi gani ambayo nimeitaja hapa lakini na *Tier...*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anatropia hata hilo nalo hata kabla Mwanasheria hajasimama inawekwa kwenye *regulations* kwa sababu hizi faini zitakuwa *reviewed*. Unapotunga sheria inaweza kukaa miaka mingi, leo Sh.50,000 unaiona ya maana lakini Sh.50,000 ya miaka 10 ijayo ni hamna kitu lakini kwa sababu inawekwa kwenye *regulations* kule wanabadili tu taratibu wanaendelea kwa *purpose* hiyo. Ukitaka iwe kwenye sheria kitu kidogo kama hiki lazima kije kurudi Bungeni tena, ndiyo maana inawekwa kwenye *regulations* na walisema kina Mheshimiwa Bashe kwamba kabla *regulations* hazijaanza kutumika basi Kamati yetu ya Sheria Ndogo itazame na Serikali Mheshimiwa Waziri kakubali. (*Makofi*)

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Kamati husika itaenda kupitia hizo kanuni, hatuna shida. Napata wasiwasi kwamba tunamuchia Waziri kutengeneza *regulations*, kila sehemu tumeona *regulation* atatunga Waziri na watu wetu wanaenda kuumia wakati sheria tumeitunga hapa Bungeni na hatujajua mwisho wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ndivyo ilivyo sina ugomvi.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 7

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anatropia Ibara ya 7.

MHE. ANATROPIA L. TEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyopitia Muswada huu nikajaribu kufanya *comparison* nimeona kama kifungu cha 7(2) ni *duplicate* ya kifungu cha 27(2) lakini ni *duplicate* ya kifungu cha 17(3). Ukiona *the content are almost the same*, kwa hiyo, naona kama hii imejirudia...

MWENYEKITI: Mheshimiwa mbona unayoyasema hukuyaandika siyaoni kwenye *schedule* yako.

MHE. ANATROPIA L. TEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza kwamba nataka hiki kifungu kiondoke kwa sababu kimekuwa *taken* na *event* kwa maana ya vifungu vingine vilivyofuatia vinaongelea kifungu hicho hicho.

MWENYEKITI: Kifungu cha 7(2), haya Mwanasheria Mkuu anasema tuondoe kifungu 7(2), anasema imerudiwa sijui wapi huko mbele.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ningemuomba atuelekeze tena kwenye hivi vifungu vingine anavyosema vinajirudia.

MWENYEKITI: Iweke sawa kwa sababu hukuwa umeviandika humu, hivyo unavyosema vinajirudia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ukienda kifungu cha 17 kinaelezea *application for licence under Tier 1 and Tier 2*. Nasoma kifungu kidogo cha (3) anasema, *the application under subsection (1) shall be accompanied with*, ameandika vitu ambavyo anapaswa kuwasilisha kwa maana ya *a certified copy of a certificate of registration or incorporation issued in terms*, hiyo (a),(b)(c) kwa maana ya *preliminary condition* za kufanya kabla ya usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukija tena kifungu 27(2) kinasema, *an application for registration shall be made to the Bank or Delegated Authority in the prescribed form and shall be accompanied with*. Kwa hiyo, hivi vyote viwili vinaonyesha mtu ili a-*qualify* kupata *licence* lazima awe na vitu hivi na *assumption* ni kwamba atakuwa ana-*run smoothly* kwa sababu ame-*meet* vigezo. Sasa kifungu cha 7(2) kinaongelea mtu tayari ame-*meet* vigezo. Ni kwa nini kifungu hicho kipo kama mtu tayari ame-*meet* vigezo vya awali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo hoja yangu ya msingi, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anatropia leo umeamua, kwa sababu hivyo vitu unavyovilinganisha wala havifanani kabisa, vina-*serve different purposes at each*, Mwanasheria Mkuu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukiri kwamba sijamuelewa vizuri sana Mheshimiwa Anatropia lakini niseme tu kifungu cha 7 anachokizungumzia kinahusiana na *microfinance service providers generic provisions*; kifungu cha 17 kinahusika na

microfinance service providers under Tiers 1, 2 and 3; na kifungu cha 27 kinahusika na microfinance service providers and Tier 4. (Makofi)

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kwa nini hajanielewa, hiki kifungu...

MWENYEKITI: Yaani siyo yeye peke yake, jitahidi tu kutueleweshwa maana wote hapa hatujaelewa.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nijitahidi wote wanielewa, nakushukuru.

MWENYEKITI: Yaani hueleweki kabisa.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kifungu cha 7(2) kinaongelea *governance ya microfinance na assumption ya governance ya microfinance* inakuwa *met* kwa sababu mtu anayepewa *licence* ame-meet vigezo ambazo ni *qualification* za awali na viambatanisha ambavyo unaona vinahitajika katika kifungu cha 17 lakini na kifungu cha 23. Kwa hiyo, *assumption* yule mtu ame-meet vigezo hahitaji kufuatwafuatwa katika kifungu cha 7(2) katika *issue ya governance*. Kama AG hatanielewa, nadhani nitamueleweshwa na tutarudhisha sheria baada ya kupata changamoto siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Haya, naruhusu ninyi mnaolewa mumuunge mkono. Mheshimiwa Anatropia si umeona nilikwambia hueleweki unajenga hoja gani. Haya Mheshimiwa Sware ulikuwa kwenye Kamati ya Bajeti tufafanulie mgongano uko wapi katika vifungu ya 7(2), 17 na 23.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Anatropia ameichukulia hiyo *section 7* inahusiana na *governance ya microfinance* kwa ujumla. Ukienda *section 17* na *23* zinachanganua ni nini huyo

business provider anatakiwa afanye. Ame-*expand*, kifungu cha 7 kinasema *governance of microfinance service provider*; kifungu cha 17 kinasimamia kwenye *application za licence*; na kifungu cha 23 kinaongelea *re-application and appeal*. Kwa hiyo, nafikiri vifungu hivi vya 17 na 23 Mheshimiwa Anatropia vimechanganua hiyo *governance* ikoje. Ahsante.

MWENYEKITI: Nakubaliana na wewe kabisa lakini hoja yake hapa sasa ni ku-*delete* kifungu cha 7(2) ndiyo maana inaleta shida. Kwa hiyo, siyo kwamba ame-*expand* anataka sasa twende kinyume cha hayo unayoyasema wakati kila kimoja kina-*serve its own purpose* mahali kilipo.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 8
Ibara ya 9

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 10

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 11

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 12

MWENYEKITI: Mheshimiwa Catherine Ruge, Ibara ya 12, tunakusikiliza, tafadhali.

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pendekezo langu la kuongeza kipengele (k)

katika kifungu kidogo cha (3) *in clause 12* kimekuwa *taken care* na Serikali na sasa kiko *reflected* kwenye *section* ya 32.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, uko vizuri eeh?

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 13

Ibara ya 14

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 15

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kichwa cha Habari cha Sehemu ya Nne

(Kichwa cha Habari kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 16

Ibara ya 17

Ibara ya 18

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 19

Ibara ya 20

Ibara ya 21

Ibara ya 22

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

Ibara ya 24

Ibara ya 25

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge mnapoona tunahoji na tunasema na Marekebisho ya Serikali, yalivyo mengi kiasi hiki maana yake Kamati ya Bajeti imefanya kazi nzuri sana lakini pia Serikali wamekuwa wasikivu sana kwa hiyo na wenyewe tunawapongeza. *(Makofi)*

Ibara ya 26

Ibara ya 27

Ibara ya 28

Ibara ya 29

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 30

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 31

Ibara ya 32

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 33

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 34

Ibara ya 35

Ibara ya 36

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 37

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 38

Ibara ya 39

Ibara ya 40

Ibara ya 41

Ibara ya 42

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 43

Ibara ya 44

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 45

Ibara ya 46

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 47

Ibara ya 48

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 49

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 50

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 51

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 52

Ibara ya 53

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 54

MWENYEKITI: Ibara ya 54, Mheshimiwa Ruge. Ngoja kidogo nitafute *ammendment* yako ili twende pamoja. Ahsante, endelea Mheshimiwa Catherine.

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Marekebisho yangu yako kwenye Ibara ya 54, yanahusu *publication of microfinance service providers*. Naomba nisome halafu nipendekeze ni nini nataka kitolewe na nini nataka kiongezwe. Nanukuu kama ifuatavyo:-

"The Bank shall, for the purpose of transparence and enhancement of public awareness, in each year or in such intervals as the Bank may determine, publish in the Gazette and in any newspaper of wide circulation, the names and full addresses of microfinance service providers."

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kuanzia kwenye maneno *"each year or in such intervals as the Bank may determine"* yaondolewe na ku-substitute for them with the words *" every three months"* kwa sababu, hii sheria ina-provide loopholes kwa maana ya kusema mwaka mzima au *in such intervals the Bank may determine*. Kwanza mwaka

ni mrefu sana lakini tukiiachia Benki Kuu mamlaka ya kuamua ni lini wa-*publicize* hawa watoa huduma ambao *license* zao zimekuwa *revoked* au wameacha ku-*operate* itakuwa siyo sawa kwa sababu *users* wanaweza wakaendelea kufanya biashara na hawa *providers* bila kujua kama bado wana-*operate legally* au *license* zao zimekuwa *revoked or not*.

MWENYEKITI: Kwa nini *specifically* miezi mitatu unayopendekeza na siyo miezi sita au tisa au kila mwezi yaani *why three months?*

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nime-*propose* miezi mitatu ili iwe *on quartely basis*, mara nne kwa mwaka ndani ya miezi 12. Kwa hiyo, nahisi ni kipindi ambacho *users* wanaweza wakapata *information*, lakini *is just a proposal* inaweza ikabadilishwa *appropriately*. (Makofi)

MWENYEKITI: Ufafanuzi wa pendekezo hilo la kila miezi mitatu taarifa itolewe na Benki Kuu. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali tunaiona hoja ya Mheshimiwa Catherine Ruge lakini miezi mitatu kama alivyosema naona kama ni mifupi kama Serikali tunapendekeza ingekwenda miezi sita, kwa hiyo, miezi sita wana-*publish*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ruge?

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nadhani ni sawa, *users* wanaweza wakapata *information* ndani ya miezi sita na wanaweza kufanya biashara na hao *providers* ambao watakuwa *publicized* kwamba *they are legally operating*. Thank you. (Makofi)

MWENYEKITI: Kwa hiyo, Mwanasheria Mkuu hapa patasomekaje?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, patasomeka kama ifuatavyo:-

"The Bank shall, for the purpose of transparency and enhancement of public awareness, in each six months or after every six months intervals, publish in the Gazette and in any newspaper of wide circulation, the names and full addresses of microfinance service providers."

MWENYEKITI: Asante sana. Maana tunatunga sheria tunataka iende hivyo hivyo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 55
Ibara ya 56
Ibara ya 57
Ibara ya 58

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 59

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 60
Ibara ya 61
Ibara ya 62
Ibara ya 63
Ibara ya 64
Ibara ya 65

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 66

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa na Serikali)

Ibara ya 66

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza
kazi yake.

SPIKA: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.
Mheshimiwa Waziri, taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika,
naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima
imepitia Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha
wa Mwaka 2018 *(The Microfinance Bill, 2018)*, kifungu kwa
kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba
taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA
MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Wajibu
wangu ni kuwahoji Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na
hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri ya kwamba tuupitishie
Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha wa Mwaka
2018 *(The Microfinance Bill, 2018)*.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

SPIKA: Nadhani walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

Tunaendelea, Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kutunga Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha kwa ajili ya Kuweka Utaratibu wa Utoaji Leseni, Kudhibiti, Kufuatilia na Kusimamia Biashara ya Huduma Ndogo za Fedha Pamoja na Mambo Yanayohusiana na Hayo *(A Bill for An Act to make provisions for the Licensing, Regulations and Supervisions of Microfinance Business and Provide for the Other Related Matters)*,

(Kusomwa Mara ya Tatu)

*(Muswada wa Sheria wa Serikali Ulisomwa
Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

SPIKA: Ahsante sana Katibu. Kwa hatua hiyo, sisi kama Bunge tumefika mahali ambapo sasa tumeshatekeleza wajibu wetu. Tumpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango na Naibu wake, Mheshimiwa Ashatu Kijaji na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na timu yote kutoka Wizara ya Fedha na sehemu nyingine ambao walihusika na Muswada huu. *(Makofi)*

Vilevile, niwapongeze sana watumishi wetu wote chini ya Katibu wa Bunge ambao wamefanya kazi kubwa sana na kwa masaa mengi kusaidia kuhakikisha kwamba jambo hili linaenda vizuri. *(Makofi)*

Nimpongeze sana Mwenyekiti na Makamu wake wa Kamati ya Bajeti na Wajumbe wa Kamati hiyo kwa ujumla wake kwa kazi kubwa sana ambayo wameifanya kwa muda

mfupi lakini wameweza kuji-*tune* na kupitia kila jambo. Huu ni mfano mzuri sana kwa Kamati nyingine za Bunge ambao mnaletewa Miswada kuipitia kwa umakini mkubwa kwa sababu tunatunga sheria. Watu wa Kamati ya Bajeti wametuonesha mfano na wengine tuufuate mfano huohuo katika kujishughulisha na kusoma, kuelewa kila kitu, kuuliza na kuhakikisha kwamba tunafanya kazi nzuri kama wenzetu wa Bajeti walivyotuongoza. *(Makofi)*

Sheria hii tulikuwa tunaihitaji sana, tunaipongeza Serikali. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuleta katika Hati ya Dharura ili tuweze kuifanyia kazi. Wengi wa wapiga kura wetu wanahusika na mambo haya na sheria hii inaenda kuwasaidia sana. Tunaomba Mheshimiwa Waziri Kanuni zake zitoke mapema iwezekanavyo, kama walivyochangia Waheshimiwa Wabunge, matatizo yanayotokana na haya mamikopo ya ajabu-ajabu yamewafika shingoni Wabunge, kama walivyosema baadhi yetu wengi wetu imebidi utumie fedha yako ili kutatua tatizo la ajabu sana. Mtu anakopeshwa shilingi milioni moja katika muda mfupi anadaiwa shilingi milioni 10, shilingi milioni 9, inabidi nyumba iwekwe rehani inataka kuuzwa, watoto wanatolewa wakae nje, tunatumaini sheria hii itaenda kurekebisha tatizo hilo kubwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya ratiba zilizoko hapa katikati ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu anazo na mimi ninazo, nawaombeni hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kutufungia shughuli zetu tuifanye saa 10.00 kamili jioni ya leo. Naomba Waheshimiwa Wabunge tuwahi mapema ili tusikilize hotuba hiyo muhimu, lakini pia kuna matangazo muhimu yatakayofuatia baada ya pale. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 10.00 kamili jioni ya leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge, inabidi tusubiri subiri kidogo naona kuna Wabunge bado wanapitapita kwenye mashine kule, tuwape nafasi waweze kufika, wakishafika tutaendelea na shughuli zetu kama kawaida.

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE

SPIKA: Taarifa ya Katibu wa Bunge.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 29(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo ya Januari, 2016, naomba kutoa taarifa kwamba, shughuli zote zilizowekwa kwenye orodha ya shughuli za Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge sasa zimemalizika.

SPIKA: Taarifa ndio hiyo Waheshimiwa Wabunge, ratiba yetu tuliyoipanga Kamati ya Uongozi ya Mkutano huu wa Kumi na Tatu, tumekamilisha shughuli zote kama ilivyopangwa, kwa umahiri mkubwa na hakuna iliyobaki tena kwa wakati.

Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

SPIKA: Sasa baada ya shughuli kukamilika ni hoja ya kuahirisha Bunge na hoja hiyo itatolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo sasa kwa heshima nimkaribishe Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu sana, utoe hoja yako.
(Makofi)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya njema na kutufikisha siku ya leo tunapohitimisha Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge lako tukufu tuliouanza siku ya Jumanne, tarehe 6 Novemba, 2018.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa umahiri mkubwa. Niwashukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kukusaidia katika kutekeleza ipasavyo majukumu ya kuliongoza Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kukamilisha shughuli zote zilizopangwa kutekelezwa kwenye Mkutano huu na kutoa michango mingi mizuri kupitia mijadala ya hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Serikali. Nitumie fursa hii kuwahakikishia kuwa, Serikali imepokea michango yenu yenye nia ya kujenga na kuimarisha utendaji wa Serikali na tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Salamu za Pole; tarehe 20 Septemba, 2018, Taifa lilipokea kwa mshtuko mkubwa taarifa za kuhuzunisha za kuzama kwa kivuko cha *MVNyerere*. Ajali hiyo mbaya iligharimu maisha ya Watanzania wapatao 227. Aidha, katika kipindi cha Septemba hadi Novemba, 2018, wapo Watanzania wenzetu waliopatwa na maafa mbalimbali ikiwemo ajali za barabarani ambazo zimegharimu maisha, kusababisha majeruhi na uharibifu mkubwa wa mali.

Mheshimiwa Spika, vilevile, mvua iliyoambatana na upepo mkali pamoja na radi iliyonyesha Mkoani Geita siku ya tarehe 17 Oktoba, 2018 ilisababisha vifo vya wanafunzi sita na Walimu wawili wa Shule ya Msingi Emaco na kujeruhi wengine 25. Hivyo, nitumie fursa hii kutuma salamu zangu za

pole kwa wale wote waliopoteza wapendwa wao. Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, Amina. Tuendeleo kuwaombea uponaji wa haraka kwa waliopata majeraha kwenye ajali mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo unafahamu Wabunge wanne walishinda chaguzi ndogo zilizoendeshwa katika Majimbo ya Monduli, Ukonga, Korogwe Vijijini na Liwale. Wabunge hao ni Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka. Hongereni sana Waheshimiwa Wabunge kwa heshima kubwa mliyoipata ya kuaminiwa na wananchi wa majimbo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wanne walioapishwa jana tarehe 15 Novemba, 2018 ambao ni Mheshimiwa James Kinyasi Millya, Mbunge wa Jimbo la Simanjiro; Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe; Mheshimiwa Ryoba Chacha Marwa, Mbunge wa Jimbo la Serengeti na Mheshimiwa Paulina Philip Gekul, Mbunge wa Babati Mjini kwa kupita bila kupingwa kwenye majimbo yao.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wapya kwa kuaminiwa na kuteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali ambao ni Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji; Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Waziri wa Kilimo; Mheshimiwa Mary Machuche Mwanjelwa, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii; Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Naibu Waziri Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Naibu Waziri wa Kilimo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwakumbusha Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri

wote kuwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wananchi wanayo matarajio makubwa kutoka kwao katika kuwaletea maendeleo. Hivyo, naomba tusiwaangushe wananchi.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama wa vyombo vya usafiri. Wakati naanza kusoma hotuba yangu nimetoa salamu za pole kutokana na ajali mbalimbali zilizohusisha vyombo vya usafiri. Ajali hizo ambazo zimegharimu maisha ya wananchi wengi ni pamoja na kuzama kwa kivuko cha *MV*Nyerere.

Mheshimiwa Spika, kufuatia ajali hiyo Serikali iliunda Tume ya kuchunguza chanzo cha ajali na kutoa mapendekezo yatakasaidia kuepuka ajali nyingine ya aina hiyo na kubainisha vyanzo vya ajali na watendaji ambao hawakutekeleza wajibu wao ipasavyo. Tayari Serikali imepokea taarifa hiyo ya Tume na inaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama barabarani bado ina changamoto nyingi licha ya takwimu kuonesha kupungua kwa matukio na vifo vinavyosababishwa na ajali hizo. Mathalan, katika mwaka 2016 matukio ya ajali za barabarani yalikuwa 9,856 ikilinganishwa na matukio 5,578 katika mwaka 2017 ambayo ni pungufu kwa matukio 4,278 sawa na asilimia 43.

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Oktoba 2018, matukio ya ajali za barabarani yalikuwa 3,209 ikilinganishwa na matukio 5,578 katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba, 2017.

Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua mbalimbali kukabiliana na matukio ya usalama barabarani. Miongoni mwa hatua hizo ni kuendesha operesheni za kuhakikisha sheria zote za usalama barabarani zinafuatwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Elimu. Katika kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa shule nchini, Serikali inapeleka

fedha za elimumsingi bila malipo moja kwa moja shuleni. Kwa mfano, katika kipindi cha Julai hadi Oktoba, 2018 shilingi bilioni 38.6 zilipelekwa katika shule za msingi na shilingi bilioni 44.6 zimepelekwa katika shule za sekondari zote nchini.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanza kutekelezwa kwa mpango wa elimumsingi bila malipo, uandikishaji wa watoto wa darasa la awali na darasa la kwanza umeimarika. Vilevile, kumekuwepo na mwenendo mzuri wa ufaulu katika mitihani ya kumaliza darasa la saba, ambapo mwaka 2016 ilikuwa wastani wa asilimia 70 na mwaka 2018 ilikuwa ni wastani wa asilimia 78. Hali hiyo, imeongeza mahitaji mbalimbali, ikiwemo miundombinu katika shule zetu zote za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na hali hiyo ya ongezeko la miundombinu, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu inaendelea na mikakati ya ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu muhimu ya shule zetu. Kwa mfano, kupitia programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (*EP4R*), shilingi bilioni 53.4 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi pamoja na za sekondari. Aidha, shilingi bilioni 9.2 zimeelekezwa katika kuimarisha miundombinu ya elimu kupitia programu ya kuboresha elimu ya shule za msingi ijulikanayo kama *EQUIP-T*.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu kwa kuweka mazingira mazuri katika mfumo mzima wa elimu nchini kwa kushirikiana na wadau wote.

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa mitihani ya Taifa kwa darasa la nne, kidato cha pili na kidato cha nne inaendelea hivi sasa. Hata hivyo, katika kipindi cha hivi karibuni kumezuka matukio ya kuvuja kwa mitihani. Naziagiza taasisi zote zinazohusika na usimamizi na uendeshaji wa mitihani ya Taifa kuhakikisha kuwa wanasimamia kikamilifu mitihani hiyo ili kuepuka udanganyifu. Itakapobainika kuwepo kwa udanganyifu wa mitihani, hatua stahiki zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria dhidi ya yeyote atakayehusika na wizi wa mitihani hiyo.

Mheshimiwa Spika, Uharibifu wa Mazingira na Vyanzo vya Maji. Nchi yetu inakabiliwa na changamoto kubwa ya uharibifu wa mazingira na ubotevu wa vyanzo vya maji. Kwa msingi huo, hatuna budi kuchukua hatua stahiki ili kudhibiti hali hiyo isiweze kuendelea. Mfano, miradi mingi ya maji nchini imekwama au kutoleta tija kutokana na uharibifu wa mazingira na vyanzo vingi vya maji kukauka.

Mheshimiwa Spika, niwasihi Waheshimiwa Wabunge wenzangu endeleeni kuwahasisha wananchi na wadau kutoa maoni yatakayosaidia kujenga na kuboresha vema sheria zinazokusudiwa kulinda mazingira yetu pamoja na vyanzo vya maji. Wananchi kwa pamoja nasi Wabunge, tukishirikiana katika kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira, vyanzo vya maji vitakuwepo vingi na huduma za maji zitatolewa mpaka vijijini. Wakati wote, Serikali iko tayari kusikiliza maoni yenu lakini pia kuyasikiliza maoni ya wananchi juu ya njia muafaka ya kuzuia uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika ziara yangu ya hivi karibuni Wilayani Lushoto, nilfarijika mno kuona jitihada kubwa zinazofanywa na wananchi wa wilaya hiyo katika kuhifadhi mazingira. Nitumie fursa hii kuwapongeza sana wananchi wa Halmashauri za Wilaya ya Lushoto na Halmashauri ya Bumbuli kwa utunzaji mzuri wa mazingira. Naziagiza Halmashauri nyingine nchini kote kuiga mfano huo mzuri wa kuhifadhi mazingira ambao nimeushuhudia Wilayani Lushoto kwenye Halmashauri za Lushoto na Bumbuli.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa Ununuzi wa Mazao Nchini; kumejitokeza hali ya kuyumba kwa bei kwa baadhi ya mazao yetu ya kimkakati, yaani kahawa, tumbaku, chai, zabibu, pamba pamoja na korosho. Hali hiyo, imesababishwa na kuyumba kwa bei za mazao hayo katika soko la dunia. Aidha, pale ambapo bei za mazao zinakuwa si nzuri au nzuri tutaendelea kutoa taarifa kwa wakulima wanaolima mazao husika ili waweze kuwa na taarifa za mara kwa mara juu ya bei na masoko ya mazao haya.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo yake mahsusi kuhusu namna bora ya uendeshaji wa biashara za mazao nchini. Kufuatia maelekezo hayo, sasa sekta binafsi hasa wafanyabiashara wanapaswa kuzingatia maslahi mapana ya wakulima na Taifa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo kwa taasisi zote za umma zinazohusika na masoko ya mazao, kama vile *TanTrade*, Bodi ya Mazao Mchanganyiko na *TMX* kutoka Wizara ya Kilimo, Wizara ya Fedha kutafuta masoko mapya na mazao yetu badala ya kutegemea wafanyabiashara pekee.

Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maamuzi yake ya kuokoa wakulima wa zao la korosho kukosa masoko ya uhakika. Korosho hizo sasa zinanunuliwa kwa bei ya Sh.3,300 na tayari malipo yameshaanza kulipwa kwa wakulima hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, niwaombe wananchi wenzangu kuendelea kutoa ushirikiano na kutambua kuwa, dhamira ya Serikali ni kuona kila mkulima ananufaika sambamba na kupata tija ya mazao anayoyalima.

Mheshimiwa Spika, Maonesho ya Viwanda na Teknolojia ya Madini; tarehe 4 Novemba, 2018 nilipata fursa ya kufungua Maonyesho ya Viwanda ya Mkoa wa Pwani ambayo yalifunguliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 29 Oktoba 2018. Aidha, tarehe 23 Oktoba, 2018 nilifungua maonesho mengine ya viwanda vidogo na biashara ndogondogo yaliyofanyika katika viwanja vya Nyakabindi, Wilayani Bariadi, Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na maonyesho yaliyofanyika Mkoani Simiyu na Pwani, tarehe 30 Septemba, 2018 nilipata pia fursa ya kufunga maonesho ya teknolojia na uwekezaji katika sekta ya madini ya dhahabu yaliyofanyika

katika Mkoa wa Geita. Maonyesho hayo yalikuwa na lengo la kuwakutanisha wadau mbalimbali wa sekta ya madini na kutangaza fursa za kiuchumi na uwekezaji zilizopo katika mnyororo mzima wa uchimbaji madini hususan dhahabu. Aidha, kupitia maonesho haya wajasiriamali wa sekta ya madini hususan wachimbaji wadogo walipata fursa ya kujifunza teknolojia bora ya uchenjuaji madini ambayo ni rafiki kwa mazingira.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji hao wadogo, pia waliweza kukutana na wataalamu wanaosimamia sekta ya madini na mabenki kwa lengo la kujifunza matumizi ya teknolojia mpya sambamba na kufahamu taratibu mbalimbali za kupata mikopo ya kuendesha shughuli zao za uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kuwapongeza Wakuu wa Mikoa ya Pwani, Simiyu na Geita kwa ubunifu wao huo. Vilevile, niwapongeze sana wazalishaji wenye viwanda na wengine wa madini pamoja na wadau wote waliohiriki kuonyesha teknolojia mbalimbali na bidhaa mpya za kilimo na madini katika maonyesho hayo maeneo yote ya mikoa hiyo mitatu.

Mheshimiwa Spika, ubunifu huu wa kufanya maonyesho ya viwanda ya Kimkoa, Kikanda na Kitaifa ni jambo muhimu sana. Maonyesho haya, yanatupa fursa ya kutangaza na kutathmini hatua tuliyofikia katika utekelezaji wa ajenda ya ujenzi wa uchumi wa viwanda na kubaini changamoto zilizopo. Vilevile, maonyesho hayo yanahamasisha wananchi wengi zaidi kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa nchi yetu kupitia viwanda. Pia, maonyesho hayo yanatoa fursa kwa wadau husika kukutana na kubadilishana utaalum, uzoefu na teknolojia mbalimbali mpya.

Mheshimiwa Spika, tarehe 22 Novemba, 2018, nitakuwa Mkoani Tabora kuzindua Jukwaa la Fursa za Biashara na Uwekezaji ambayo itakuwa ni nafasi za kutangaza fursa zao Mkoani Tabora ili kukaribisha Wawekezaji

kufanya shughuli zao za Uwekezaji Mkoani Tabora. Napenda kuielekeza mikoa mingine kuiga mifano hiyo ya Mikoa ya Pwani, Simiyu na Geita pamoja na Tabora ili kuhamasisha wananchi na wadau wengine kushiriki ipasavyo katika ujenzi wa viwanda na kuleta teknolojia mpya za viwanda na sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia, kuwataka wananchi kujenga utamaduni wa kutumia bidhaa zetu zinazozalishwa hapa nchini ili kulinda viwanda vyetu na kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Bunge; naomba kuhitimisha kwa kuainisha kwa uchache yaliyojiri katika Mkutano huu wa Bunge na mazingatio ya Serikali:-

Mheshimiwa Spika, Maswali na Majibu; idadi ya maswali 120 ya msingi na 272 ya nyongeza yaliulizwa Bungeni kuhusu kero na utekelezaji wa miradi mbalimbali. Aidha, katika utaratibu wa maswali kwa Waziri Mkuu, niliulizwa maswali ya msingi 12 na la nyongeza moja. Hii ni ishara kuwa Wabunge wana hamu ya kuona changamoto zikipata ufumbuzi na wana hamu ya kuona huduma na maendeleo yanawafikia wananchi kwa wakati. Pamoja na majibu yaliyotolewa, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali itaongeza kasi katika kutekeleza na kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kadri hali ya uchumi itakavyokuwa inaruhusu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imewasilisha mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti ya mwaka 2019/2020. Bunge lako Tukufu, lilipata fursa ya kujadili kwa kina Mpango na Mwongozo wa Bajeti kwa muda wa siku tano. Katika siku hizo, tulipokea michango mbalimbali muhimu itakayotusaidia sana katika utendaji wa kazi ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, michango hiyo pia itasaidia katika kuboresha mpango wa bajeti ya mwaka ujao na hivyo, kuondoa changamoto za wananchi na kuakisi dhamira ya

Serikali ya Awamu ya Tano ya kuleta maendeleo ili kuifikisha nchi katika uchumi wa kati. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu mwendeele kuishauri Serikali kwenye sekta zote za uzalishaji, hususan kilimo, uvuvi, madini, mifugo, viwanda na utalii.

Mheshimiwa Spika, Miswada ya Serikali; Tarehe 15 Novemba, 2018 Serikali iliwasilisha Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha wa mwaka 2018 (*The Microfinance Act, 2018*) ambao umesomwa kwa hatua zake zote na kupitishwa na Bunge lako Tukufu, ukisubiri kibali cha Mheshimiwa Rais ili kuwa sheria kamili.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sekta ndogo ya fedha haikuwa na udhibiti wa kutosha. Hali hiyo ilisababisha kuwepo uendeshaji usio rasmi wa shughuli mbalimbali za kifedha. Mathalan, taasisi zinazochukua amana, vikundi vya fedha vya jamii na wakopeshaji binafsi.

Mheshimiwa Spika, shughuli hizo ambazo nyingi ziliendeshwa katika utaratibu usio rasmi ziliwaitea athari mbalimbali wananchi ikiwemo kupoteza mali zao, nyumba, magari na rasilimali nyingine zilizokuwa zimewekwa kama amana kwenye taasisi hizo. Aidha, baadhi ya watu wasiokuwa waaminifu wamekuwa wakitumia mwanya wa kutokuwepo udhibiti wa kutosha kwenye sekta hiyo ndogo ya fedha kuendesha vitendo mbalimbali vya kihalifu ikiwemo na utakatishaji fedha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hizo, Serikali iliamua kutunga Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 kwa lengo la kuongeza udhibiti wa sekta hiyo ndogo ya fedha na kuiwezesha kuchangia ipasavyo katika kuimarisha uchumi wa nchi na kulinda mali na fedha za wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Wataalam wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Waziri wa Katiba

na Sheria, kupitia kwa Mwanasheria Mkuu, Kamati ya Bajeti ya Wabunge na Waheshimiwa Wabunge kwa kuridhia Muswada huu baada ya kupata fursa ya kuchangia mawazo mbalimbali kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Miswada mingine mitano imesomwa kwa mara ya kwanza ambayo ni:

(i) Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa mwaka 2018;

(ii) Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa mwaka 2018;

(iii) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania wa mwaka 2018;

(iv) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Nchi Kavu wa mwaka 2018; na

(v) Muswada wa Kutunga Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira wa mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, Maazimio ya Kuridhia Mikataba na Itifaki za Kimataifa. Katika Mkutano huu wa Bunge maazimio yafuatayo yaliwasilishwa na kuridhiwa na Bunge lako:-

(i) Azimio la Kuridhia Itifaki ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Kulinda Hatimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea;

(ii) Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Matumizi ya Silaha za Kibaiolojia na Sumu; na

(iii) Mapendekezo ya Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika. Bunge limeridhia kwa kauli moja kupitisha azimio hili. Serikali inawataka Watanzania wote watumie

takwimu sahihi kutoka vyanzo sahihi ili kukidhi mahitaji na kuondoa mkanganyiko kwa matumizi ya takwimu zisizokuwa sahihi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba nitumie nafasi hii kwenu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kuwatakia heri, maandalizi mema na ushindi kwa Timu yetu ya Taifa ya Mpira wa Miguu (*Taifa Stars*), wakati wa mchezo wake dhidi ya timu ya Taifa ya Lesotho tarehe 18 Novemba, 2018 ili kuwania tiketi ya kufuzu kwa michuano ya AFCON nchini Cameroon mwaka 2019. Safari ya kuelekea Cameroon iko nyeupe, sasa ni zamu yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kwenu Waheshimiwa Wabunge kuwatakia heri pia maandalizi mema na ushindi kwa Timu ya Bunge *Sports Club*, ambayo mwaka huu inakwenda kucheza nchini Burundi ikiwakilisha Bunge letu, lakini pia na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye michezo hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu kuwa mwaka huu wa 2018, timu yetu ya Bunge *Sports Club* itarudi na makombe yote. Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge, tunaitakia Timu yetu ya Bunge *Sports* mafanikio mema na mrudi mkiwa na makombe ili tuweze kuyasherehekea hapa nyumbani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za dhati kwa Katibu wa Bunge, watendaji na maafisa wengine wa Serikali kwa kuratibu na kufanikisha shughuli za Mkutano huu kama zilivyopangwa. Nataka nitumie nafasi hii pia kuwashukuru Madereva mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Serikali waliowezesha kuwaleta hapa Bungeni na kuendelea na shughuli zote za hapa Bungeni. Ni matumaini yangu kwamba, Madereva hawa Mungu atawalinda na kuwaongoza kuwarudisha Viongozi mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kurudi makwao kwa mapumziko na kuendelea na kazi kwenye Majimbo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) limetangaza kuwa Maulid ya kuadhimisha mazazi ya Mtume Muhammad (*Swalla Allahu Alayh Wasallam*) kitaifa itasomwa usiku wa Jumatatu tarehe 19 Novemba, 2018 Korogwe, Mkoani Tanga. Napenda kutumia fursa hii kuwatakia waumini wote wa dini ya Kiislamu sherehe njema za maadhimisho ya Maulid. Aidha, kwa waumini wote wa Kikristo, nawatakia sikukuu njema ya Krismasi tarehe 25 Desemba, 2018. Vilevile, nawatakia Watanzania wote heri ya mwaka mpya wa 2019 ambao utakuja hivi karibuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumanne, tarehe 29 Januari, 2019 saa tatu asubuhi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono na imeungwa mkono na Bunge zima, Tunakushukuru sana Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri, hotuba fupi, hotuba ya uhakika, tunakushukuru sana, sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa vile ni hoja aliyoitoa Waziri Mkuu, hoja ya kuahirisha Bunge lazima tuifanyie uamuzi, kwa hiyo nitawahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge na mimi niwashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kazi nzuri ambayo tumefanya inayoingia katika kumbukumbu ya nchi yetu ya mkutano ambao hautajirudia tena katika historia ya nchi hii Mkutano wetu wa Kumi na Tatu wa Bunge hili la

Kumi na Moja, toka tupate uhuru, tumefanya kazi zetu zote kama ulivyopangwa kwa ufanisi mkubwa na kama nilivyosema tumemaliza kwa wakati ule ule tuliopanga.

Ni Taasisi chache zinaendeshwa kwa umahiri mkubwa kama Bunge, wakati mwingine tusipojisemea wenyewe nani atasema bwana, maana Bunge ndiyo taasisi ambayo ikipanga jambo linaanza saa tatu ni saa tatu, litakwisha saa fulani ni palepale, linaanza tarehe fulani na shughuli ni hizi na litakwisha tarehe fulani pale pale. Kwa hiyo, ni lazima tujivune kidogo kwamba kwa kupanga na kutekeleza na sisi Bunge tumo na sifa hii inawaendea ninyi wenyewe Waheshimiwa Wabunge wote, wengine wote wangepanga hivi hivi nadhani tungesogea kwa haraka zaidi, watuige. *(Makofi)*

Naomba niwashukuru sana wasaidizi wangu hapa mezani Mheshimiwa Tulia Ackson, Mheshimiwa Chenge, Mheshimiwa Zungu, Mheshimiwa Najma kwa kunisaidia kila wakati hapa mezani, bila wao peke yangu nisingeweza, kwa hiyo nawashukuru sana. Pia niwashukuru Wenyeviti wote wa Kamati na Makamu Wenyeviti, Waheshimiwa Mawaziri wote, wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu asanteni sana. Vile vile nakushukuru sana *Chief Whip* kwa jinsi ambavyo unatupatia kila aina ya ushirikiano, bila ushirikiano wako mambo mengi yangekwama, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Nami niwatakie kila la kheri katika sikukuu ya Maulid inayokuja keshokutwa, tusherehekee salama, lakini pia Krismasi na mwaka mpya, niwatakie krismasi njema na mwaka mpya mwema. Niwaombe sana madereva wetu watupeleke salama na taratibu. Ukimwona dereva wako anakimbia sana mrudishe mwambie hapa barabara inasema hamsini hapa inasema 80, mbona upo 130.

Waheshimiwa Wabunge, tafadhali tusishabikie mwendo kasi, mwendo kasi umeruhusiwa Dar es Salaam tu, tena kwenye ile barabara maalum, sisi twende mwendo wa kawaida utafika tu unapokwenda. Mwendo kasi unaweza usifikie unapokwenda, hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa

twende kwa mwendo wa kawaida. Kama safari yako ni ndefu, basi ianze mapema kuliko kuanza umechelewa halafu mnakimbiakimbia barabarani hovy, ni jambo ambalo si jema hata kidogo.

Niwatakie kila la kheri Waheshimiwa Wabunge ambao hivi sasa wapo kitandani, mahali tofauti tofauti mahospitalini, wakiwa wanaumwa, tunawatakia kila la kheri wapate uponyaji mwema na niwaombe wale mnaosafiri hasa katika kipindi hiki cha Krismasi na mwaka mpya ambao mnakwenda nje ya nchi na sehemu mbalimbali ya nchi, tunao utaratibu pale Ofisi ya Spika hapa au Dar es Salaam, pita pale pata kikaratasi chetu kidogo, tuandikie pale si kwamba ni cha ruhusa, lakini inatusaidia ukituambia kwamba umekwenda mahali fulani, unaweza ukapata matatizo huko unapokwenda, kumbuka ni jukumu letu vilevile kusaidiana na mamlaka zozote zile utakapokuwa kuhakikisha unarudi salama ukipata tatizo.

Hata hivyo, ukiona hutaki kufanya hivyo, basi puyanga tu, lakini ukipata shida huko, nasi tutasema hatujui huyu mtu aliko kwa hiyo, hayo ni mambo yake binafsi, lakini ukituachia maandishi pale kidogo, ukatutajia nchi unayokwenda, hatutaki kujua unakwenda kufanya nini, lakini *at least* tuwe tunaweza hata kukutafuta *in case* kuna tatizo Fulani, ndugu yetu kuna hili la wapiga kura huku, inasaidia sana.

Pia tunamshukuru sana Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ni kupitia ushirikiano wake mkubwa sana kwa Bunge hili, ndiyo maana mnaona mambo yanakwenda na hasa mambo yanayohusu utaratibu. Mheshimiwa Waziri wa Fedha akinizinguazingua kidogo basi mambo yanakuwa mazuri kupitia Mheshimiwa Rais wetu. Kwa kweli anatupa kila aina ya ushirikiano, hivyo tuna kila sababu ya kumshukuru. (*Makofi*)

Basi baada ya maelezo hayo sasa naomba Waheshimiwa Wabunge tusimame ili turuhusu *Brass Band* waweze kutuongoza katika kuimba Wimbo wa Taifa. Wimbo wa Taifa, tafadhali

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(Hapa Wimbo wa Taifa uliimbwa)

SPIKA: Ahsanteni sana *Brass Band*, ahsanteni sana JKT Makutupora. Sasa naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi mwakani 2019 mwezi Januari kwa tarehe ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameitaja. Ahsanteni sana.

(Saa 10.36 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 29 Januari, 2019, Saa Tatu Asubuhi)